TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA

# MTAALA WA SHULE YA JUNIA

# KISWAHILI

## GREDI YA TISA

DRAFT

Toleo la Kwanza 2024

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa mtaala huu kwa njia yoyote ile bila idhini, kwa maandishi, ya mchapishaji.

**ISBN: 978-9914-43-434-7**

Umechapishwa na kutolewa na Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya.

DRAFT

## DIBAJI YA WAZIRI WA ELIMU

Serikali ya Kenya imejitolea kuhakikisha kuwa malengo ya sera kuhusu elimu, mafunzo na utafiti yanatimiza malengo ya Katiba ya Kenya ya 2010, Ruwaza ya Kenya 2030, Sera ya Mtaala ya Kitaifa 2019, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa na Mikataba ya Kikanda na ya Kimataifa ambayo Kenya ni mshirika. Katika kutimiza lengo la Elimu ya Msingi, Wizara ya Elimu imefanikiwa kutekeleza hatua kwa hatua Mtaala wa Kiumilisi katika viwango vya Chekechea, Shule ya Msingi na katika Daraja ya Awali ya Shule za Upili.

Utekelezwaji wa Mtaala wa kiumilisi, unahusisha, kuangalia mara kwa mara vile unaendelea kutekelezwa ili kutathmini utekelezwaji wake. Miaka mitano baada ya kutekelezwa kwake, tathmini tamati ya utekelezwaji ulifanywa katika shule za msingi ili kubainisha ufanisi wake kama inavyopendekezwa katika Utaratibu wa Mtaala wa Elimu ya Msingi (BECF). Serikali ya Kenya iliunda Tume ya Rais ya Elimu ya kushughulikia masuala mbalimbali, yanayoathiri sekta ya elimu nchini mwaka wa 2022. Tume hii ilitoa mapendekezo mbalimbali, yaliyochangia marekebisho ya mtaala. Mapendekezo ya tume hii, ripoti za tathmini, tathmini tamati zilizofanywa, mapendekezo kutoka kwa washikadau, na wale wanaotekeleza mtaala yalisababisha hatua ya kufanya marekebisho katika mtaala pamoja na kuchunguza upya masomo yaliyopendekezwa.

Mitaala ya Gredi ya 9 inaendeleza umilisi walioupata wanafunzi kufikia mwisho wa Gredi ya 8. Aidha, inatoa fursa kwa wanafunzi kuendelea kutalii na kukuza uwezo wao wanapojiandaa kujiunga na Daraja ya Juu ya Shule za Upili.

Mtaala huu unaeleza Malengo ya Elimu ya Kitaifa, kauli kiini, matokeo ya kijumla na maalum yanayotarajiwa kwa kila somo pamoja na mada na mada ndogo. Mtaala huu pia unabainisha mapendekezo ya shughuli za ujifunzaji, Maswali Dadisi yaliyopendekezwa, umilisi wa kimsingi unaokuzwa, masuala mtambuko, maadili, shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji na vigezo na viwango vya kuzingatia katika kutathmini.

Ni matumaini yangu kuwa, mashirika yote ya serikali na wadau wengine wa elimu watatumia mtaala kuandaa utekelezaji fanifu na wenye tija wa Mtaala wa Kiumilisi.

**MHE. EZEKIEL OMBAKI MACHOGU, CBS**
**WAZIRI WA ELIMU**,
**<u>WIZARA YA ELIMU</u>**

DRAFT

## DIBAJI YA KATIBU MKUU

Wizara ya Elimu imetekeleza Mtaala wa Kiumilisi ulioanza mwaka wa 2019. Gredi ya 9 ndiyo kiwango cha mwisho cha Daraja ya Awali ya Shule za Upili katika mpangilio mpya wa elimu.

Mtaala wa Gredi ya 9 unaendeleza utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi kutoka Gredi ya 8. Mtaala wa Gredi ya 9 pia inaendeleza utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi kutoka Gredi ya 7.Sifa kuu ya daraja hii ni mtaala mpana unaomwezesha mwanafunzi kutalii talanta, hamu na uwezo wake kabla ya kuchagua mkondo wa masomo katika Daraja ya Juu ya Shule za Upili. Hili ni muhimu sana katika kutimiza ruwaza na lengo la mabadiliko ya mtaala yanayoendelea kama ilivyoelezwa katika Mswada Elekezi Nambari 1 wa mwaka 2019 wenye mada: *Kuelekea kufikia Elimu Bora, Faafu na Jumuishi na Mafunzo kwa Maendeleo Endelevu Nchini Kenya*. Mswada huu unafafanua mabadiliko kutoka kwa mtaala unaolenga kupokeza maarifa hadi mtaala unaolenga *Kukuza uwezo wa kila Mwanafunzi.*

Kwa hivyo, mtaala wa Gredi ya 9 unakusudiwa kuimarisha ukuaji wa mwanafunzi katika umilisi wa kimsingi wa Mtaala wa Kiumilisi ambao ni: mawasiliano na ushirikiano, uwazaji kina na utatuzi wa matatizo, ubunifu, uraia, ujuzi wa kidijitali, hamu ya ujifunzaji na kujiamini.

Mtaala huu unatoa mapendekezo ya shughuli za ujifunzaji husishi na tofautishi kuambatana na mada ndogo mbalimbali na vipengele vingine vya Mtaala wa Kiumilisi. Mtaala pia unapendekeza nyenzo za kufundishia pamoja na mbinu anuwai za kutathminia. Inatarajiwa kuwa mtaala huu utawaongoza walimu kikamilifu kuwaelekeza wanafunzi kufikia matokeo yanayotarajiwa katika Gredi ya 9 na kuwaandaa kuingia katika Daraja ya Juu Shule za Upili. Vilevile, ni matumaini yangu kuwa walimu watautumia mtaala huu kuufanya ujifunzaji kuwa wa kuvutia, kuchangamsha na wenye kufurahisha.

**DKT. BELIO KIPSANG', CBS**
**KATIBU MKUU**
**IDARA YA SERIKALI YA ELIMU YA MSINGI**
**WIZARA YA ELIMU**

DRAFT

## SHUKRANI

Sheria Nambari 4 ya 2013 (iliyorekebishwa 2019) ya Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya (KICD) inaipa mamlaka Taasisi kukuza mitaala na nyenzo za utekelezaji mtaala kwa elimu ya msingi na taasisi za elimu na mafunzo. Mchakato wa ukuzaji mtaala wa kiwango chochote cha elimu huhusisha utafiti wa kina, ulinganishi wa kimataifa na uhusishaji mkubwa wa wadau. Kupitia kwa mchakato uliopangwa kikamilifu na wa mashauriano, KICD ilibuni Mtaala wa Kiumilisi (CBC) kama ilivyoelezwa katika Utaratibu wa Mtaala wa Elimu ya Msingi (BECF) 2017,ambao unaitikia mahitaji ya karne ya 21 na matamanio yanayoelezwa katika Katiba ya Kenya ya 2010, Ruwaza ya 2030, Itifaki ya Jumuia ya Afrika Mashariki pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa.

KICD hupata ufadhili kutoka kwa Serikali ya Kenya ili kuwezesha ufikiaji kikamilifu wa majukumu na utekelezaji wa mipango ya serikali na sekta za Wizara ya Elimu. Taasisi pia inapata msaada kutoka kwa washirika wa maendeleo unaolenga miradi mahususi. Mtaala wa Gredi ya 9 uliofanyiwa marekebisho, umeandaliwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia mpango wa *Kenya Primary Education Equity in Learning Programme (KPEELP*) ulio chini ya uelekezi wa Wizara ya Elimu. Kwa hivyo, Taasisi inatoa shukrani za dhati kwa msaada kutoka kwa Serikali ya Kenya kupitia Wizara ya Elimu na washirika wengine wa maendeleo kwa sera na msaada wa mali na mikakati. Taasisi inatoa shukrani za kipekee kwa Waziri wa Elimu, Katibu Mkuu katika Idara ya Serikali ya Mafunzo ya Awali na Elimu ya Msingi.

Tungependa kuwashukuru wakuza mitaala wa KICD na wafanyakazi wengine, walimu wote na wakufunzi walioshiriki kama wanajopo katika ukuzaji wa mitaala. Nashukuru pia Mashirika Huru ya Serikali (SAGAs) na wawakilishi wa wadau mbalimbali kwa michango yao katika kuuandaa Mtaala wa Gredi ya 9. Kwa mintarafu hii, tunatambua msaada wa Afisa Mkuu Mtendaji wa Tume ya Kuwaajiri Walimu (TSC) na Afisa Mkuu Mtendaji wa Baraza la Kitaifa la Mitihani nchini Kenya (KNEC) kwa usaidizi wao katika mchakato mzima wa kuuandaa mtaala. Mwisho, tunamshukuru Mwenyekiti wa Baraza la Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya (KICD) na wanachama wengine wa Baraza kwa uelekezi wao wa mara kwa mara katika mchakato huu.

Tunawahakikishia walimu wote, wazazi na wadau wengine kuwa mtaala huu utaelekeza ipasavyo utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi katika Gredi ya 9 na uandaaji wa wanafunzi kwa Daraja ya Juu Shule za Upili.

**PROF. CHARLES O. ONG'ONDO, PhD, MBS**
**MKURUGENZI/OFISA MTENDAJI MKUU**
**<u>TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA</u>**

DRAFT

**YALIYOMO**

DIBAJI YA WAZIRI WA ELIMU ... iii
DIBAJI YA KATIBU MKUU ... iv
SHUKRANI ... v
YALIYOMO ... vi
MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA ... viii
MGAO WA VIPINDI ... x
KAULI KIINI ... xv
MATOKEO YA KIJUMLA YANAYOTARAJIWA KATIKA SHULE YA JUNIA ... xvi
MWONGOZO WA KUTUMIA VITABU VYA KUSOMA KATIKA SHULE YA JUNIA ... xvii
1.0 USAFI WA MAZINGIRA ... 1
2.0 MAZOEZI YA VIUNGO VYA MWILI ... 9
3.0 UTUNZAJI WA WANYAMA ... 17
4.0 UTUNZAJI WA MALIASILI ... 25
5.0 MITAZAMO HASI YA KIJINSIA ... 33
6.0 USALAMA BARABARANI ... 41
7.0 HUDUMA KATIKA ASASI ZA KIJAMII ... 50
8.0 MISUKOSUKO YA KIJAMII ... 58

DRAFT

9.0 MATUMIZI YA VIFAA VYA KIDIJITALI KATIKA BIASHARA ........ 68
10.0 KUKABILIANA NA MSONGO WA MAWAZO ........ 76
11.0 HAKI ZA KIBINADAMU ........ 85
12.0 MAGONJWA YANAYOTOKANA NA MIENENDO YA MAISHA ........ 95
13.0 MSHIKAMANO WA KIJAMII ........ 103
14.0 MATUMIZI YA KODI ........ 111
15.0 MAADILI YA KITAIFA ........ 120
MWONGOZO WA VIGEZO NA VIWANGO VYA KUTATHMINIA ULIOPENDEKEZWA ........ 128
MUHTASARI WA MBINU ZA KUTATHMINI, NYENZO ZA KUFUNDISHIA NA MAPENDEKEZO YA SHUGHULI NYINGINE ZILIZORATIBIWA ZA UJIFUNZAJI ........ 141

DRAFT

## MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA

Elimu nchini Kenya inatakiwa:

1. **Kukuza na kustawisha utaifa, uzalendo na kuendeleza umoja wa kitaifa**

   Nchini Kenya kuna jamii zenye mila, dini na tamaduni mbalimbali lakini tofauti hizi hazifai kuzitenganisha. Lazima waweze kuishi na kutangamana kama Wakenya. Elimu ina jukumu kuu la kuwezesha vijana kujenga hisia za uzalendo na utaifa kwa kuondoa mivutano na kukuza mielekeo chanya ya kuheshimiana itakayowezesha jamii kuishi pamoja kwa utangamano na kujenga uzalendo ili kuchangia uhai wa taifa.

2. **Kukidhi mahitaji ya kijamii, kiuchumi, kiteknolojia na viwanda yanayochangia maendeleo ya kitaifa**

   Elimu inafaa kuwaandaa vijana wa nchi kutekeleza wajibu wenye umuhimu katika maisha nchini.

   a) **Mahitaji ya kijamii**

      Elimu nchini Kenya lazima iwatayarishe vijana kwa mabadiliko ya mielekeo na mahusiano ambayo yanahitajika kwa maendeleo ya haraka ya uchumi wa kisasa. Kuna uwezekano wa kuwa na mapinduzi kimyakimya ya kijamii kutokana na maendeleo ya haraka ya usasa. Elimu inapaswa kuwasaidia vijana kujirekekebisha kutokana na mabadiliko haya.

   b) **Mahitaji ya kiuchumi**

      Elimu nchini Kenya inafaa kukuza raia walio na stadi, maarifa, ujuzi na sifa za kibinafsi zinazohitajika kuhimili maendeleo ya kiuchumi. Kenya inajenga uchumi huru na wa kisasa ambao unahitaji wafanyakazi wa kutosha, walio na maarifa yanayohitajika na wa humu nchini.

   c) **Mahitaji ya kiteknolojia na ya kiviwanda**

      Elimu nchini Kenya inafaa kuwapa vijana stadi na mielekeo inayohitajika kwa maendeleo ya kiviwanda. Kenya inatambua mabadiliko ya haraka ya kiviwanda na kiteknolojia yanayofanyika, hasa katika ulimwengu ulioendelea. Tunaweza kuwa sehemu ya maendeleo haya ikiwa mfumo wetu wa elimu utalenga kimakusudi maarifa, stadi na mielekeo itakayotayarisha vijana kwa mabadiliko ya yanayoendelea ulimwenguni.

.

DRAFT

3. **Kutoa nafasi ya kujiendeleza na kujitosheleza**
Elimu inapaswa kumwezesha mtu kutambua, kukuza na kuimarisha kipawa chake ili aweze kujiendeleza na kujitosheleza. Inafaa kuwawezesha watoto kukuza uwezo wao. Kipengele muhimu cha maendeleo ya kibinafsi ni ujenzi wa tabia ifaayo.

4. **Kuwawezesha wananchi kuimarisha maadili na amali za kijamii na kidini**
Elimu inakusudiwa kukuza maarifa, stadi na mielekeo itakayoimarisha upataji wa maadili na kuwasaidia watoto kukua wakiwa wenye nidhamu, wanaojitegemea na raia wakamilifu.

5. **Kuimarisha usawa wa kijamii na uwajibikaji**
Usawa wa kijamii kwa mfano usawa wa kijinsia huimarika watu wa jamii na jinsia zote wanapopata elimu sawa. Elimu inafaa ikuze usawa wa kijamii na uwajibikaji wa kijamii kutokana na mfumo wa elimu unaowezesha fursa sawa ya elimu kwa wote. Inafaa kuwapa watoto wote fursa mbalimbali na zilizo na changamoto kwa mazoezi ya pamoja na ushirika katika huduma za kijamii bila kujali jinsia, uwezo au mazingira ya kijiografia.

6. **Kukuza uthamini wa tamaduni mbalimbali nchini Kenya**
Elimu inafaa kutoa nafasi kwa wanaosoma kuelewa, kuthamini, kukuza na kudumisha tamaduni faafu na kudondoa zile potofu kulingana na jamii ya wakati uliopo ili kujenga jamii ya kisasa.

7. **Kuimarisha utambuzi wa uhusiano wa kimataifa na kukuza mwelekeo chanya kwa mataifa mengine**
Kenya kama nchi mojawapo ya jamii ya kimataifa inakusudia elimu iwaelekeze Wakenya kutambua na kuthamini mahusiano ya kimataifa kwa kuzingatia mikataba, uwajibikaji, haki na manufaa yanayoambatana na ushirika huo.

8. **Kustawisha mwelekeo chanya kuhusu afya bora na uhifadhi wa mazingira**
Elimu inakusudiwa kujenga mielekeo ifaayo miongoni mwa vijana kuhusu udumishaji wa afya bora na mazingira kwa kujiepusha na mienendo inayoweza kudhuru afya ya mwili na akili. Elimu inafaa pia kuimarisha mielekeo chanya kuhusu ukuzaji na uhifadhi wa mazingira. Inafaa kuwaelekeza vijana wa Kenya kukubali haja ya mazingira safi.

DRAFT

**MGAO WA VIPINDI**

| | **Somo** | **Vipindi kwa wiki (Dakika 40 kwa kipindi)** |
|---|---|---|
| 1. | English | 5 |
| 2. | Kiswahili/KSL | 4 |
| 3. | Mathematics | 5 |
| 4. | Integrated Science | 5 |
| 5. | Social Studies | 4 |
| 6. | Religious Studies | 4 |
| 7. | Pre-Technical Studies | 4 |
| 8. | Agriculture and Nutrition | 4 |
| 9. | Creative Arts and Sports | 5 |
| | Pastoral/Religious Instructional Programme | 1* |
| | **Jumla** | **40 +1*** |

DRAFT

**MUHTASARI WA MADA NA MADA NDOGO**

| Mada | Mada Ndogo | Idadi ya Vipindi Vilivyopendekezwa |
|---|---|---|
| **KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA** | 1.1.1 Kusikiliza na Kujibu; Mjadala | 2 |
| | 2.1.1 Kusikiliza kwa Kina; sauti **/b/** na **/mb/** | 2 |
| | 3.1.1 Semi; tashbihi, sitiari na methali | 2 |
| | 4.1.1 Semi: Vitendawili na nahau | 2 |
| | 5.1.1 Ufahamu wa Kusikiliza | 2 |
| | 6.1.1 Kusikiliza kwa Kufasiri | 2 |
| | 7.1.1 Kusikiliza kwa Kutathmini | 2 |
| | 8.1.1 Uzungumzaji wa Kushawishi | 2 |
| | 9.1.1 Kusikiliza kwa Kina: Sauti **/j/** na **/nj/** | 2 |
| | 10.1.1 Mazungumzo: Malumbano ya Utani | 2 |
| | 11.1.1 Uzungumzaji katika Sherehe | 2 |
| | 12.1.1 Ufahamu wa Kusikiliza | 2 |
| | 13.1.1 Mazungumzo: Mawaidha | 2 |
| | 14.1.1 Mazungumzo: Mawaidha | 2 |
| | 15.1.1 Kusikiliza kwa Kutathmini | 2 |
| **KUSOMA** | 1.2.1 Kusoma kwa Ufahamu: Simulizi | 2 |
| | 2.2.1 Kusoma kwa Mapana: Matini ya kujichagulia | 2 |
| | 3.2.1 Kusoma kwa Kina: Ushairi | 2 |

| | | |
|---|---|---|
| | 4.2.1 Kusoma kwa Ufasaha | 2 |
| | 5.2.1 Kusoma kwa Ufahamu | 2 |
| | 6.2.1 Kusoma kwa Kina: Ushairi | 2 |
| | 7 .2.1 Ufupisho | 2 |
| | 8.2.1 Kusoma kwa Kina: Ushairi | 2 |
| | 9.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**:** Kifungu cha Kushawishi | 2 |
| | 10.2.1 Kusoma kwa Kina: Ushairi | 2 |
| | 11.2.1 Kusoma kwa Mapana: Matini ya kujichagulia | 2 |
| | 12.2.1 Kusoma kwa Ufasaha | 2 |
| | 13.2.1 Kusoma kwa Kina: Ushairi | 2 |
| | 14.2.1 Kusoma kwa Ufahamu | 2 |
| | 15.2.1 Ufupisho | 2 |
| **KUANDIKA** | 1.3.1 Viakifishi: Koloni na Semi koloni | 2 |
| | 2.3.1 Insha za Kiuamilifu: Barua ya Kirafiki | 2 |
| | 3.3.1 Insha za Kubuni: Masimulizi | 2 |
| | 4.3.1 Insha za Kubuni: Masimulizi | 2 |
| | 5.3.1 Insha za Kiuamilifu: Shajara | 2 |
| | 6.3.1 Insha za Kubuni: Methali | 2 |
| | 7.3.1 Insha za Kubuni: Maelezo | 2 |
| | 8.3.1 Viakifishi: Mabano na Kistari Kifupi | 2 |
| | 9.3.1 Insha za Kubuni: Masimulizi | 2 |

DRAFT

| | | |
|---|---|---|
| | 10.3.1 Barua ya Kuomba Kazi | 2 |
| | 11.3.1 Insha za Kubuni: Maelezo | 2 |
| | 12.3.1 Hotuba ya Kushawishi | 2 |
| | 13.3.1 Insha za Kubuni: Maelezo | 2 |
| | 14.3.1 Insha za Kiuamilifu: Shajara | 2 |
| | 15.3.1 Kujibu Baruapepe | 2 |
| **SARUFI** | 1.4.1 Vihusishi: Vihusishi vya Mahali na Vihusishi vya Wakati | 2 |
| | 2.4.1 Vihusishi: Vihusishi vya **-a** Unganifu na Vihusishi vya Sababu | 2 |
| | 3.4.1 Vihusishi**:** Vihusishi Vilinganishi na Kihusishi **na** | 2 |
| | 4.4.1 Nyakati na Hali: **-ki-** ya masharti na **-ka-** ya kufuatana kwa vitendo | 2 |
| | 5.4.1 Hali za Masharti: Hali ya masharti **-nge-** na Hali ya masharti **-ngali-** | 2 |
| | 6.4.1 Vielezi**:** Vielezi vya Namna na Vielezi vya Wakati | 2 |
| | 7.4.1 Vielezi: Vielezi vya Mahali na Vielezi vya Idadi | 2 |
| | 8.4.1 Ngeli na Upatanisho wa Kisarufi: Ngeli ya **U-ZI** na Ngeli ya **YA-YA** | 2 |
| | 9.4.1 Ngeli na Upatanisho wa Kisarufi: Ngeli ya **LI, KU, PA-KU-MU** | 2 |

DRAFT

| | | |
|---|---|---|
| | 10.4.1 Vinyume vya Vihusishi | 2 |
| | 11.4.1 Mnyambuliko wa Vitenzi: Kauli ya: Kutendana, Kutendeana na Kutendesha | 2 |
| | 12.4.1 Aina za Sentensi: Sentensi tata | 2 |
| | 13.4.1 Ukanushaji: Hali ya masharti **-nge-, -ngali-** na **-ki-** | 2 |
| | 14.4.1 Udogo na Ukubwa wa Nomino | 2 |
| | 15.4.1 Usemi Halisi na Usemi wa Taarifa | 2 |
| **Jumla ya vipindi** | | 120 |

**Kumbuka:** Idadi ya vipindi vilivyopendekezwa kwa kila mada ndogo vinaweza kuwa vichache au vingi kutegemea na muktadha.

DRAFT

**MATOKEO YA KIJUMLA YANAYOTARAJIWA KATIKA KIWANGO CHA KATI CHA ELIMU YA MSINGI**

Kufikia mwisho wa kiwango cha kati cha elimu, mwanafunzi aweze:

1. kutumia ujuzi wa kusoma na kuandika, ujuzi wa kuhesabu na kufikiri kimantiki ifaavyo katika kujieleza
2. kuwasiliana kikamilifu katika miktadha mbalimbali
3. kudhihirisha ujuzi wa kijamii, pamoja na tunu za kiimani na kimaadili kwa ajili ya mahusiano mema
4. kutalii, kubadilisha, kusimamia na kutunza mazingira ifaavyo kwa ajili ya ujifunzaji na maendeleo endelevu
5. kufanya usafi, kufuata kanuni zifaazo za usafi na lishe ili kuimarisha afya
6. kudhihirisha mienendo ya kimaadili na kuonyesha uraia mwema kama wajibu wa kiraia
7. kuonyesha ridhaa kwa mirathi mingi na tofauti ya kitamaduni nchini ili kuleta mshikamano wa kimahusiano
8. kudhibiti masuala mtambuko katika jamii ifaavyo
9. kutumia ujuzi wa kidijitali ifaavyo kwa madhumuni ya mawasiliano na ujifunzaji.

**KAULI KIINI**

Somo la Kiswahili litampa mwanafunzi wa Shule ya Junia umilisi katika shughuli za kila siku. Umilisi huu utajengea haiba na uwezo wake wa kuwasiliana na kuhusiana katika jamii, kitaifa na kimataifa. Aidha, litamwendeleza kielimu na kumwandaa kwa ulimwengu wa kazi. Somo hili litampa mwanafunzi hamasa ya kumudu na kufurahia lugha na fasihi kwa kuzihusisha na tajriba na mazingira yake. Hali kadhalika, litampa mwanafunzi maarifa ya kijamii na kitamaduni. Mwanafunzi ataweza kujieleza na vilevile kupata fursa ya kutoa huduma kwa jamii.

## MATOKEO YA KIJUMLA YANAYOTARAJIWA KATIKA SHULE YA JUNIA

Kufikia mwisho wa Shule ya Junia, mwanafunzi aweze:

1. kujieleza ipasavyo kwa kutumia lugha ya Kiswahili kwa njia ya maandishi na mazungumzo
2. kuwasiliana ipasavyo katika miktadha mbalimbali ya kijamii
3. kujenga desturi ya kusoma na kufasiri maandishi kwa ufasaha
4. kutumia lugha kiubunifu kusimulia na kuandika tungo mbalimbali
5. kushiriki katika shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji
6. kutumia teknolojia ipasavyo katika ujifunzaji na mawasiliano ili kukuza ujuzi wa kidijitali
7. kutumia maadili yanayohitajika maishani kupitia stadi za lugha ya Kiswahili
8. kufurahia na kuthamini lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi, ya taifa na kimataifa.

DRAFT

**MWONGOZO WA KUTUMIA VITABU VYA KUSOMA KATIKA SHULE YA JUNIA**

**Lengo la Vitabu vya Kusoma katika Shule ya Junia**

Utanzu ulioteuliwa wa kusomwa katika Gredi ya Tisa ni wa Diwani ya Mashairi. Matokeo yanayotarajiwa:

i. kukuza jadi ya usomaji miongoni mwa wanafunzi jambo ambalo ni muhimu miongoni mwa wanafunzi katika maisha yao ya ujifunzaji,
ii. kuwaandaa wanafunzi kusoma fasihi katika somo la Kiswahili katika mkondo wa Sayansi ya Jamii katika Shule ya Juu,
iii. kuwatanguliza wanafunzi katika vipengele vya kimsingi vya fasihi ambavyo ni muhimu katika maisha ya kila siku tukijua kwamba wengine watasoma fasihi katika Shule ya Juu.

**Kufunza vitabu vya Kusoma katika Shule ya Junia**

**Wanafunzi katika shule ya Junia:**

i. wataongozwa kusoma vitabu mbalimbali ili kuwapa nafasi ya kuingiliana na dhana na stadi katika mtaala. Hali hii itawaweka katika hali ya kupata stadi za kuzungumza, kusikiliza, kusoma, kuandika, sarufi mwanzoni,
ii. wanatarajiwa kuingiliana na tanzu mbalimbali ili kuwa na uzoevu wa dhana za kimsingi za fasihi ili kujiburudisha na pia kukuza mazoea ya usomaji,
iii. hawapaswi kushirikishwa katika uhakiki wa kazi za fasihi kwa undani.

Ni muhimu kukumbuka kuwa ni vitabu tu vilivyoidhinishwa na KICD vinavyopaswa kusomwa kulingana na viwango lengwa.

**Tathmini ya Vitabu vya Kusoma**

Kama inavyopendekezwa katika mtaala, tathmini endelevu na tamati haipaswi kuegemea vitabu vyovyote teule. Hii ni kwa sababu vitabu hivi vya kusoma SIO vitabu teule vya fasihi au *setbooks* kama vinavyojulikana. Tathmini inapaswa kuwa wazi na ya vipengele vya kimsingi kulenga dhana za kimsingi kama zinavyoelekezwa katika mtaala. Zaidi ya hayo, tathmini inapaswa kufanywa kwa njia ambayo kila mwanafunzi atakuwa na nafasi sawa bila kujali ni kitabu gani ambacho mwanafunzi amesoma.

DRAFT

**1.0 USAFI WA MAZINGIRA**

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **1.1.1 Kusikiliza na Kujibu**<br><br>*Mjadala*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza mjadala,<br>b) kutambua vipengele vya kuzingatia katika kuchangia mjadala,<br>c) kushiriki mjadala kwa kuzingatia vipengele vifaavyo katika kusikiliza na kuchangia mijadala,<br>d) kuchangamkia kushiriki katika mijadala ya miktadha mbalimbali. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza mjadala,<br>• kutambua vipengele vya kuzingatia katika kuchangia mjadala,<br>• kusikiliza au kutazama mjadala kuhusu suala lengwa katika kifaa cha kidijitali,<br>• kueleza vipengele vya kusikiliza na kuchangia mjadala vilivyozingatiwa katika mjadala aliosikiliza,<br>• kushiriki mjadala kuhusu suala lengwa akiwa na wenzake akizingatia vipengele vifaavyo vya mjadala. | Je, unazingatia nini wakati wa kusikiliza na kuchangia mjadala? |

DRAFT

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia ipasavyo katika shughuli za ujifunzaji kuhusu kusikiliza na kujibu mjadala.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kama vile redio na kanda za sauti katika kusikiliza mijadala mbalimbali.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotumia mitindo anuwai kuwashawishi wenzake katika mjadala kuhusu suala lengwa.
- Kujiamini: mwanafunzi anapochangia mjadala ipasavyo.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapoheshimu zamu ya wengine katika mazungumzo.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapovitunza vifaa vya kidijitali anavyotumia katika kusikiliza au kutazama mjadala.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

- Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anaposhiriki katika mjadala kuhusu suala lengwa.
- Elimu ya afya ya kujikinga: mwanafunzi anaposhiriki katika mjadala kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusikiliza na kujibizana aliyojifunza katika somo la Kiwahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafi wa mazingira na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.2 Kusoma** | **1.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>*Kifungu cha Simulizi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kudondoa habari mahususi katika kifungu cha simulizi,<br>b) kupanga matukio yanavyofuatana katika kifungu cha simulizi,<br>c) kufanya utabiri na ufasiri kutokana na kifungu cha simulizi,<br>d) kueleza maana ya msamiati kama ulivyotumiwa katika kifungu cha simulizi,<br>e) kuchangamkia kujibu maswali ya ufahamu ili kukuza uelewa wa habari. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua habari mahususi katika kifungu cha simulizi kuhusu suala lengwa,<br>• kudondoa habari mahususi katika kifungu cha simulizi,<br>• kupanga matukio yanavyofuatana katika kifungu cha simulizi,<br>• kutabiri matukio katika kifungu cha simulizi kutokana na picha au matukio,<br>• kufasiri habari kutokana na kifungu cha simulizi,<br>• kueleza maana ya maneno au msamiati kulingana na matumizi yake kimuktadha,<br>• kutunga sentensi akitumia msamiati wa suala lengwa kwa usahihi na kuwasomea wenzake au kuwatumia mtandaoni ili wazitolee maoni. | Unafanya nini ili kupata habari zilizo katika kifungu cha simulizi kwa usahihi? |
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapochangia kikamilifu na kushirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji kuhusu usomaji wa kifungu cha simulizi. | | | | |

DRAFT

| |
|---|
| • Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo kutunga sentensi sahihi.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia msamiati wa suala lengwa. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapokubaliana na maoni ya wenzake na kushirikiana nao katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kutunza kifaa cha kidijitali. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anaposoma matini kuhusu suala lengwa.<br>• Elimu ya afya ya kujikinga: mwanafunzi anaposoma matini kuhusu suala lengwa na kuzingatia ujumbe. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kwa ufahamu, na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafi wa mazingira na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi yaliyopendekezwa |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| **1.3 Kuandika** | **1.3.1 Viakifishi**<br><br>• *Koloni*<br>• *Semi koloni*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua alama ya koloni na semi koloni katika matini,<br>b) kueleza matumizi ya koloni na semi koloni katika matini,<br>c) kutumia alama ya koloni na semi koloni ipasavyo katika matini,<br>d) kufurahia matumizi yafaayo ya alama ya koloni na semi koloni katika matini mbalimbali. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua alama ya koloni na semi koloni katika sentensi au vifungu kwenye matini andishi au za kidijitali,<br>• kueleza matumizi ya koloni na semi koloni katika matini,<br>• kusahihisha kifungu ambacho hakijatumia alama ya koloni na semi koloni ipasavyo,<br>• kuandika daftarini mwake au kwenye kifaa cha kidijitali, sentensi au kifungu kifupi kuhusu suala lengwa na masuala mengine kwa kutumia alama ya koloni na semi koloni ipasavyo,<br>• kuwasomea wenzake kazi yake au kuwasambazia kwenye mtandao ili waitolee maoni,<br>• kumweleza mzazi au mlezi wake kuhusu sentensi au vifungu alivyoandika vilivyo na matumizi mbalimbali ya alama za koloni na | 1. Je, alama ya koloni hutumiwa wapi katika maandishi?<br>2. Je, alama ya semi koloni hutumiwa vipi katika maandishi? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | semi koloni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika kusahihisha vifungu walivyoandika.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kuandika kifungu na kukisambaza mtandaoni.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika vifungu vyenye matumizi yafaayo ya alama za koloni na semi koloni.

**Maadili:**

- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

- Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa.
- Elimu ya afya ya kujikinga: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya uakifishaji aliyojifunza katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafi wa mazingira na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.4 Sarufi** | **1.4.1 Vihusishi**<br><br>• *Vihusishi vya Mahali*<br>• *Vihusishi vya Wakati*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vihusishi vya mahali na vya wakati katika matini,<br>b) kutumia vihusishi vya mahali na vya wakati ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia matumizi yafaayo ya vihusishi vya mahali na vya wakati katika matini mbalimbali. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua vihusishi vya mahali na vya wakati kutoka kwa kapu maneno, mti maneno, chati, vitabu au katika tarakilishi,<br>• kutambua vihusishi vya mahali na vya wakati katika sentensi au vifungu kwenye vitabu au tarakilishi kwa kuvipigia mstari au kuvikolezea wino,<br>• kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kutumia vihusishi vya mahali na vya wakati ipasavyo,<br>• kutunga sentensi au vifungu vifupi kwa kutumia vihusishi vya mahali na vya wakati akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la usafi wa mazingira,<br>• kumsomea mzazi au mlezi wake | 1. Je, ni wakati gani tunatumia vihusishi vya mahali?<br>2. Je, vihusishi vya wakati vinatumika wakati gani? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | sentensi au vifungu alivyotunga ili amtolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji kuhusu vihusishi husika.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kutambua vihusishi vya mahali na wakati.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia vihusishi vya mahali na wakati.

**Maadili:**
- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika mchakato wa ujifunzaji wa vihusishi vya mahali na vya wakati.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala Mtambuko:**
- Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa.
- Elimu ya afya ya kujikinga: mwanafunzi anapoandika sentensi au kifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia viwakilishi mbalimbali.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vihusishi vya mahali na vya wakati na yale amejifunza kuhusu dhana hizo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafi wa mazingira na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture.

DRAFT

## 2.0 MAZOEZI YA VIUNGO VYA MWILI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **2.1.1 Kusikiliza kwa Kina**<br><br>*Sauti /**b**/ na /**mb**/*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutamka sauti **/b/** na **/mb/** ipasavyo ili kuzitofautisha kimatamshi,<br>b) kutamka vitanzandimi vyenye sauti /**b/** na **/mb/** ipasavyo,<br>c) kuunda vitanzandimi vyepesi vyenye sauti /**b**/ na **/mb/**,<br>d) kuchangamkia matamshi bora ya sauti /**b/** na **/mb/** katika mazungumzo ya kawaida. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua sauti **/b/** na **/mb/** katika maneno na vifungu,<br>• kusikiliza na kutamka vitanzandimi vyepesi vinavyohusisha matamshi ya sauti **/b/** na **/mb/** katika kifaa cha kidijitali kama vile simu, redio,<br>• kubuni vitanzandimi vyepesi vinavyohusisha sauti **/b/** na **/mb/**,<br>• kuwasomea wenzake vitanzandimi alivyobuni ili wamtolee maoni. | Kutamka maneno yenye sauti **/b/** na **/mb/** ipasavyo kuna umuhimu gani? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kusikiliza vitanzandimi vyenye sauti lengwa.
- Ubunifu: mwanafunzi anapobuni vitanzandimi vyepesi akitumia maneno yenye sauti lengwa.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotamka vitanzandimi ipasavyo yenye sauti lengwa.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapowasomea wenzake vitanzandimi alivyobuni kwa kuhusisha matamshi bora ya sauti lengwa.

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika mchakato wa ujifunzaji.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kutunza kifaa cha kidijitali anachotumia.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Masuala Mtambuko**:<br>Afya ya mtu binafsi: mawanafunzi anapobuni vitanzandimi akizingatia suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matamshi bora aliyojifunza katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mazoezi ya viungo vya mwili na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Creative Arts and Sports. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.2 Kusoma** | **2.2.1 Kusoma kwa Mapana**<br><br>*Matini ya kujichagulia*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kufafanua ujumbe wa matini aliyosoma,<br>b) kutambua msamiati uliotumiwa katika matini ya kujichagulia,<br>c) kutumia ipasavyo msamiati unaotokana na matini aliyosoma,<br>d) kujenga mazoea ya kusoma matini mbalimbali za kujichagulia. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kuteua matini kuhusu suala linalomvutia,<br>• kusoma matini aliyojichagulia na kutambua vipengele vyake muhimu,<br>• kufafanua ujumbe wa matini aliyosoma kwa ufupi,<br>• kutambua msamiati uliotumiwa katika matini aliyojichagulia kwa kutumia kamusi kutafuta maana za maneno asiyoyajua,<br>• kutunga sentensi akitumia msamiati katika matini aliyoisoma na kuziwasilisha darasani ili mwenzake wazitolee maoni,<br>• kusakura mtandaoni na kujichagulia matini ya kusoma kisha afafanue maana ya msamiati na ujumbe katika matini hiyo. | 1. Unazingatia nini unapojichagulia matini ya kusoma?<br>2. Ni mambo gani unayofaa kufanya unaposoma matini ya kujichagulia? |
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na mwenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutunga sentensi kutokana na msamiati wa matini ya kujichagulia.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia msamiati aliojifunza.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojichagulia matini ya kusoma na kutafuta maana za maneno asiyoyajua kwenye kamusi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura mtandaoni na kujichagulia matini ya kusoma. | | | | |

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili**:<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kutafuta na kusoma matini.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi akitumia msamiati aliojifunza. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anaposoma matini ya kujichagulia kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha kusoma kwa mapana katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu usomaji huo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi  anaweza kuhusisha suala la mazoezi ya viungo vya mwili na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Creative Arts and Sports. |

DRAFT

<table>
<tr><th>Mada</th><th>Mada Ndogo</th><th>Matokeo Maalum Yanayotarajiwa</th><th>Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji</th><th>Swali Dadisi Lililopendekezwa</th></tr>
<tr><td>2.3 Kuandika</td><td>2.3.1 Insha za Kiuamilifu<br><br>Barua ya Kirafiki<br><br>(Vipindi 2)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua ujumbe unaoafiki katika kujibu barua ya kirafiki,<br>b) kueleza lugha inayofaa katika kujibu barua ya kirafiki,<br>c) kufafanua muundo unaofaa katika kujibu barua ya kirafiki,<br>d) kujibu barua ya kirafiki akizingatia ujumbe, lugha na muundo ufaao,<br>e) kujenga mazoea ya kujibu barua ya kirafiki katika maisha ya kila siku.</td><td>Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua ujumbe unaoafiki anapojibu barua ya kirafiki,<br>• kueleza lugha inayofaa kujibu barua ya kirafiki<br>• kujadili muundo wa kujibu barua ya kirafiki akishirikiana na wenzake,<br>• kujibu barua ya kirafiki akizingatia ujumbe, lugha na muundo ufaao,<br>• kusomea wenzake barua aliyoiandika ili waitolee maoni.</td><td>Unazingatia nini unapojibu barua ya kirafiki?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika katika shughuli za ujifunzaji kuhusu kujibu barua ya kirafiki.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapoandika barua ya kujibu barua ya kirafiki.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapowasomea wenzake barua aliyoandika.</td></tr>
</table>

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika mchakato wa ujifunzaji.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anapoandika barua kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa barua ya kirafiki katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu uandishi huo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mazoezi ya viungo vya mwili na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Creative Arts and Sports. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.4 Sarufi** | **2.4.1 Vihusishi**<br><br>• *Vihusishi vya -a Unganifu*<br>• *Vihusishi vya Sababu*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vihusishi vya **-a** unganifu na vya sababu katika matini,<br>b) kutumia vihusishi vya **-a** unganifu na vya sababu ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia matumizi yafaayo ya vihusishi vya -a unganifu na vya sababu katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua vihusishi vya **-a** unganifu na vya sababu kutoka kwa kapu maneno, mti maneno, chati au katika tarakilishi,<br>• kutambua vihusishi vya **-a** unganifu na vya sababu katika sentensi au vifungu kwenye vitabu au tarakilishi kwa kuzipigia mstari au kuzikolezea wino,<br>• kutunga sentensi au vifungu vifupi kwa kutumia vihusishi vya **-a** unganifu na vya sababu akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la mazoezi ya viungo vya mwili,<br>• kumsomea mzazi au mlezi wake sentensi au vifungu alivyotunga ili amtolee maoni. | Vihusishi vya a unganifu na vya sababu vinatofautianaje? |
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji kuhusu vihusishi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kutambua vihusishi vya -a unganifu na vya sababu.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu suala lengwa akitumia vihusishi vya -a unganifu na vya sababu.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomtajia mzazi au mlezi wake vihusishi vya -a unganifu na vya sababu katika | | | | |

DRAFT

| |
|---|
| mazingira ya nyumbani. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anapotunga sentensi au kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vihusishi katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu dhana hiyo katika somo la English.<br>• English: somo hili pia linashughulikia.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mazoezi ya viungo vya mwili na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Creative Arts and Sports . |

DRAFT

## 3.0 UTUNZAJI WA WANYAMA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **3.1.1 Semi**<br><br>• *Tashbihi*<br>• *Sitiari*<br>• *Methali*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya tashbihi, sitiari na methali ili kuzipambanua,<br>b) kutambua tashbihi, sitiari na methali katika matini ya fasihi simulizi,<br>c) kueleza matumizi ya tashbihi, sitiari na methali katika matini ya fasihi simulizi,<br>d) kutumia tashbihi, sitiari na methali katika uwasilishaji wa tungo za fasihi simulizi,<br>e) kuchangamkia matumizi ya tashbihi, sitiari na methali katika tungo za fasihi simulizi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya tashbihi, sitiari na methali,<br>• kutambua tashbihi, sitiari na methali kutoka kwenye tungo simulizi, kapu la semi, au kifaa cha kidijitali,<br>• kutumia vifaa vya kidijitali kusakura matumizi ya tashbihi, sitiari na methali katika tungo za fasihi simulizi,<br>• kujadili na mwenzake matumizi ya tashbihi, sitiari na methali alizotafiti mtandaoni,<br>• kushiriki katika uwasilishaji wa tashbihi, sitiari na methali,<br>• kujadiliana na mzazi au mlezi wake kuhusu tashbihi, sitiari na methali katika jamii yake. | 1. Tunatumia mbinu gani za lugha katika kuwasilisha tungo za fasihi simulizi?<br>2. Kwa nini tunatumia tashbihi, sitiari na methali kuwasilisha tungo za fasihi simulizi? |

DRAFT

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji kuhusu tashbihi, sitiari na methali.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapowasilisha tashbihi, sitiari na methali kwa mitindo anuwai.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojadiliana na mzazi wake kuhusu tashbihi, sitiari na methali katika jamii yake.<br>• Uraia: mwanafunzi anapojifunza kuhusu tashbihi, sitiari na methali za jamii yake na kuzithamini.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kusikiliza tashbihi, sitiari na methali na kuzichanganua. |
| **Maadili:**<br>• Uzalendo: mwanafunzi anapoelezea tashbihi, sitiari na methali za jamii yake na kuzionea fahari.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia darasani.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake kutambua tashbihi, sitiari na methali kuhusu suala lengwa.<br>• Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapowazia kuhusu umuhimu wa wanyama. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha tungo za fasihi simulizi katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu tungo za fasihi simulizi hizo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la utunzaji wa wanyama na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Agriculture. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.2 Kusoma** | **3.2.1 Kusoma kwa Kina**<br><br>*Ushairi*<br>• *Sifa za ushairi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya shairi ili kulitofautisha na tungo nyingine,<br>b) kujadili sifa za ushairi kama utanzu wa fasihi andishi,<br>c) kueleza sifa za ushairi katika shairi,<br>d) kufurahia kuchambua ushairi kama utungo wa fasihi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutafiti maana ya shairi vitabuni au mtandaoni ili kulitofautisha na tungo nyingine,<br>• kujadili na wenzake sifa za ushairi kama utanzu wa fasihi andishi,<br>• kusoma mashairi katika diwani iliyoteuliwa na mwalimu na kueleza sifa za ushairi katika mashairi hayo,<br>• kuwasomea wenzake sifa alizotambua katika mashairi aliyoyasoma ili wamtolee maoni. | 1. Je, shairi ulilowahi kusoma lilikuwa linazungumzia nini?<br>2. Unavutiwa na nini unaposoma shairi? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapowasomea wenzake shairi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowasomea wenzake sifa za shairi alilosoma.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura mtandaoni shairi na kuchambua sifa zake.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anaposoma shairi na kuchambua sifa zake.

**Maadili:**
- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.

DRAFT

| |
|---|
| • Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anaposoma shairi kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha usomaji wa kina katika somo la Kiswahili na usomaji huo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la utunzaji wa wanyama na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Agriculture. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.3 Kuandika** | **3.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>*Masimulizi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya kufafanulia ujumbe wa insha ya masimulizi,<br>b) kufafanua ujumbe wa insha ya masimulizi kupitia kwa utangulizi, kiini na hitimisho,<br>c) kufafanua ujumbe wa insha ya masimulizi kupitia kwa wahusika,<br>d) kuandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia ujumbe na muundo ufaao,<br>e) kufurahia kufafanua ujumbe wa insha ya kusimulia ili kufanikisha maelezo. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua vipengele vya kufafanulia ujumbe wa simulizi,<br>• kusoma kielelezo cha insha ya masimulizi na kufafanua ujumbe kupitia kwa utangulizi, kiini na hitimisho,<br>• kusoma kielelezo cha insha ya masimulizi kwenye matini za aina mbalimbali na kufafanua ujumbe kupitia kwa wahusika,<br>• kuandika insha ya masimulizi daftarini mwake au katika kifaa cha kidijitali akizingatia ufafanuzi ufaao wa ujumbe kupitia kwa utangulizi ,kiini, hitimisho n wahusika,<br>• kuwasomea wenzake insha aliyoandika darasani au awasambazie kwenye vifaa vya kidijitali ili waitolee maoni, | Unafanya nini unaposimulia jambo ili ujumbe wako upate kueleweka zaidi? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusahihisha insha ya masimulizi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusambazia insha.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha ya masimulizi akizingatia ufafanuzi ufaao wa ujumbe kupitia kwa wahusika.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuandika insha na kuwasomea wenzake. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anapoandika insha ya kubuni kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa insha ya masimulizi katika somo la Kiswahili na uandishi huo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la utunzaji wa wanyama na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Agriculture. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.1 Vihusishi**<br><br>• *Vihusishi Vilinganishi*<br>• *Kihusishi **na***<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vihusishi vilinganishi na kihusishi **na** katika matini,<br>b) kutumia vihusishi vilinganishi na kihusishi **na** ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia kutumia vihusishi vilinganishi na kihusishi **na** katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kuchopoa vihusishi vilinganishi na kihusishi **na** katika kapu maneno, mti maneno, chati au katika tarakilishi,<br>• kutambua vihusishi vilinganishi na kihusishi **na** katika sentensi au vifungu kwenye vitabu au tarakilishi kwa kuzipigia mstari au kuzikolezea wino,<br>• kutunga sentensi au vifungu kwa kutumia vihusishi vilinganishi na kihusishi **na** akizingatia suala lengwa na masuala mtambuko mbalimbali,<br>• kumtajia mzazi au mlezi wake kihusishi **na** na vihusishi vilinganishi katika mazingira ya nyumbani. | Vihusishi vilinganishi na kihusishi **na** huchangia vipi katika mawasiliano? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji kuhusu aina za vihusishi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kutambua vihusishi vilinganishi na kihusishi **na**.

DRAFT

| |
|---|
| • Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua vihusishi vilinganishi na kihusishi **na** katika matini na kuvitungia sentensi sahihi na vifungu.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomtajia mzazi au mlezi wake vihusishi vilinganishi na kihusishi **na** katika mazingira ya nyumbani. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anapoandika sentensi au kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vihusishi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la utunzaji wa wanyama na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Agriculture. |

DRAFT

**4.0 UTUNZAJI WA MALIASILI**

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji** | **Maswali Dadisi yaliyopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **4.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **4.1.1 Semi**<br><br>• *Vitendawili*<br>• *Nahau*<br><br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya vitendawili na nahau ili kuipambanua,<br>b) kutambua vitendawili na nahau katika matini,<br>c) kufafanua umuhimu wa vitendawili na nahau katika fasihi simulizi,<br>d) kutumia nahau ipasavyo katika mawasiliano,<br>e) kuwasilisha vitendawili kwa kuzingatia vipengele vya uwasilishaji wake,<br>f) kuchangamkia matumizi ya nahau na uwasilishaji wa vitendawili katika tungo za fasihi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya vitendawili,<br>• kueleza maana ya nahau,<br>• kutambua vitendawili na nahau mbalimbali katika matini ya fasihi simulizi na kueleza maana zake,<br>• kutafiti mtandaoni au maktabani umuhimu wa vitendawili na nahau,<br>• kujaza nafasi katika sentensi kwa kutumia nahau mwafaka,<br>• kutunga sentensi kwa kutumia nahau ipasavyo,<br>• kujadili vipengele vya uwasilishaji wa vitendawili akiwa na wenzake,<br>• kuwawasilishia wenzake vitendawili kwa kuzingatia vipengele vya uwasilishaji wa vitendawili,<br>• kushirikiana na mzazi au mlezi wake kutambua vitendawili na nahau katika jamii yake. | 1. Unazingatia nini unapowasilisha vitendawili?<br>2. Kwa nini tunatumia nahau katika mawasiliano? |

DRAFT

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika kuwasilisha vitendawili mbalimbali.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kuwasilisha vitendawili na nahau katika kikundi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotega na kutegua vitendawili, anapotoa maana za nahau na kuchangia katika kikundi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi wake kutambua vitendawili na nahau kutoka kwa jamii yake.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika majadiliano ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika kuwasilisha vitendawili na nahau katika kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

- Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anaposhiriki katika kutega na kutegua vitendawili na wenzake kuhusu suala la maliasili katika mazingira yake.
- Elimu ya kifedha: mwanafunzi anaposhiriki katika kutega na kutegua vitendawili na wenzake kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana za vitendawili na nahau katika somo la Kiswahili na dhana hizo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la utunzaji wa maliasili na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.2 Kusoma** | **4.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya kuzingatia katika kusoma kwa ufasaha,<br>b) kusoma kifungu cha nathari akizingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu cha nathari akizingatia kasi ifaayo,<br>d) kusoma kifungu cha nathari akizingatia kiwango kifaacho cha sauti,<br>e) kusoma kifungu cha nathari akizingatia ishara za mwili zifaazo,<br>f) kujenga mazoea ya kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua vipengele vya kuzingatia katika kusoma kwa ufasaha,<br>• kusoma kifungu cha nathari akizingatia matamshi bora,<br>• kusoma kifungu cha nathari akizingatia kasi ifaayo (*maneno sahihi yasiyopungua 110 kwa dakika*),<br>• kusoma kifungu cha nathari akizingatia kiwango kifaacho cha sauti,<br>• kusoma kifungu cha nathari akizingatia ishara za mwili zifaazo,<br>• kusakura kifungu cha nathari mtandaoni na kuwasomea wenzake kwa ufasaha,<br>• kumsomea mzazi au mlezi wake kifungu cha nathari kwa ufasaha ili akitolee maoni. | Je, unaposoma kifungu chochote unazingatia mambo gani? |



DRAFT

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika kusoma kwa ufasaha.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anaposoma kifungu kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya usomaji.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusakura kifungu cha nathari. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu wenzake wakisoma kifungu.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.<br>• Umoja: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kujadili vipengele vya kuzingatia katika kusoma kwa ufasaha. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa hasa kuhusu suala la maliasili katika mazingira yake.<br>• Elimu ya kifedha: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa na kuwazia kuhusu matumizi ya maliasili.<br>• Umaskini: mwanafunzi anapowazia jinsi matumizi yafaayo ya maliasili yanawezesha kupunguza umaskini. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha kusoma kwa ufasaha katika somo la Kiswahili na usomaji huo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la utunzaji wa maliasili na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.3 Kuandika** | **4.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>*Masimulizi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na mandhari ili kuibanisha,<br>b) kujadili lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na mandhari katika insha ya masimulizi,<br>c) kuandika insha ya masimulizi akizingatia lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na mandhari,<br>d) kufurahia kuandika insha za masimulizi akizingatia lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na uchoraji wa mandhari ufaao ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua vipengele vya lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na mandhari katika masimulizi kwenye matini andishi au za kidijitali,<br>• kusoma vielelezo vya insha ya kubuni kwenye matini za kimaandishi au za kidijitali na kubainisha lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na mandhari,<br>• kuandika insha ya masimulizi kuhusu suala lengwa akitumia vipengele vifaavyo vya lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na mandhari ili kujenga taswira zifaazo,<br>• kuwasomea wenzake insha aliyoandika kuhusu suala lengwa ili wachanganue lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na mandhari. | Je, unazingatia vipengele vipi unapoandika insha ya masimulizi? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika kuchanganua lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na uchoraji wa mandhari katika insha.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha kwa kuzingatia lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na uchoraji wa mandhari ufaao.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapowasomea wenzake insha aliyoandika na kuwataka wachanganue lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na uchoraji wa mandhari.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuwasomea wenzake insha aliyoandika. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa hasa kuhusu suala maliasili katika mazingira yake.<br>• Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa na kuwazia kuhusu matumizi ya maliasili.<br>• Umaskini: mwanafunzi anapowazia jinsi matumizi yafaayo ya maliasili yanawezesha kupunguza umaskini. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa insha ya masimulizi katika somo la Kiswahili na uandishi huo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la utunzaji wa maliasili na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4 .4 Sarufi** | **4.4.1 Nyakati na Hali**<br><br>• ***-ki-*** *ya masharti*<br>• ***-ka-*** *ya kufuatana kwa vitendo*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua **-ki-** ya masharti na **-ka-** ya kufuatana katika matini,<br>b) kutumia **-ki-** ya masharti na **-ka-** ya kufuatana ipasavyo katika matini,<br>c) kujenga mazoea ya kutumia ipasavyo **-ki-** ya masharti na **-ka-** ya kufuatana kwa vitendo ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua **-ki-** ya masharti na **ka-** ya kufuatana kwa vitendo katika matini mbalimbali,<br>• kuchagua sentensi zinazoashiria matumizi ya hali ya **-ki-** na **ka-** ya kufuatana kwa vitendo kutokana na mchanganyiko wa sentensi kutoka katika vitabu, tarakilishi, chati kwa kuzikolezea wino au kuzipigia mstari,<br>• kutunga sentensi au kifungu kifupi kuonyesha matumizi ya hali ya -**ki**- na **ka-** ya kufuatana kwa vitendo akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la utunzaji wa maliasili, | 1. **-ki-** ya masharti hutumiwa wakati gani katika sentensi?<br>2. **-ka-** ya kufuatana kwa vitendo hutumiwa wakati gani katika sentensi? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za darasani.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kutambua hali ya masharti **-ki-** na hali ya kufuatana kwa vitendo **-ka-.**
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kwa kutumia hali ya masharti -**ki-** na kufuatana kwa vitendo **-ka-.**

DRAFT

| |
|---|
| • Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua hali ya masharti **–ki-** na kufuatana kwa vitendo **-ka-** kisha kuzitungia sentensi sahihi. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa hasa kuhusu suala maliasili katika mazingira yake.<br>• Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa na kuwazia kuhusu matumizi ya maliasili.<br>• Umaskini: mwanafunzi anapowazia jinsi matumizi yafaayo ya maliasili yanawezesha kupunguza umaskini. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya nyakati na hali katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la utunzaji wa maliasili na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Agriculture. |

DRAFT

## 5.0 MITAZAMO HASI YA KIJINSIA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **5.1.1 Ufahamu wa Kusikiliza**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya ufahamu wa kusikiliza,<br>b) kujadili kanuni za ufahamu wa kusikiliza,<br>c) kujadili vipengele vya ufahamu wa kusikiliza,<br>d) kushiriki katika ufahamu wa kusikiliza akizingatia vipengele vyake,<br>e) kuchangamkia kushiriki katika kusikiliza kwa ufahamu ili kukuza stadi ya kusikiliza. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya ufahamu wa kusikiliza,<br>• kujadili na wenzake kanuni za ufahamu wa kusikiliza,<br>• kujadili na wenzake vipengele vya ufahamu wa kusikiliza,<br>• kusikiliza ufahamu kuhusu suala lengwa kutoka kwa mwalimu au mgeni mwalikwa na kujibu maswali,<br>• kusikiliza matini kuhusu suala lengwa katika chombo cha kidijitali na kujibu maswali. | 1. Je, ni mambo gani unayozingatia ili kupata ujumbe unaposikiliza matini?<br>2. Je, kusikiliza kwa ufahamu kuna faida zipi? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapoeleza ujumbe aliopata kutokana na ufahamu wa kusikiliza.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki shughuli ya kusikiliza kwa ufahamu ili kupata ujumbe.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza matini ya ufahamu.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapofasiri ujumbe kutokana na ufahamu wa kusikiliza.

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Uadilifu:  mwanafunzi anapowasikiliza wasemaji kwa makini.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia katika mazungumzo.<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika mchakato wa ujifunzaji.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kufasiri ujumbe katika kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Masuala ya kijinsia: mwanafunzi anaposikiliza ufahamu kuhusu suala lengwa.<br>• Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anaposikiliza ufahamu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusikiliza kwa ufahamu katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mitazamo hasi ya kijinsia na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Studies. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.2 Kusoma** | **5.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kudondoa habari mahususi katika kifungu cha ufahamu,<br>b) kufanya utabiri na ufasiri kutokana na kifungu cha ufahamu,<br>c) kueleza maana ya msamiati kulingana na kifungu cha ufahamu,<br>d) kuchangamkia kusoma kwa ufahamu ili kukuza uelewa wa habari. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kusoma kifungu cha ufahamu na kudondoa habari mahususi,<br>• kueleza habari za kifungu cha ufahamu kwa ufupi,<br>• kufanya utabiri na ufasiri kutokana na kifungu cha ufahamu,<br>• kuchopoa msamiati wa suala lengwa kwenye kapu maneno, mti maneno, chati au kwenye vitabu,<br>• kueleza maana ya msamiati kulingana na muktadha wa matumizi katika matini,<br>• kutumia maneno hayo kutunga sentensi sahihi kisha kumsomea wenzake ili wamtolee maoni. | 1. Kwa nini tunasoma kifungu cha ufahamu?<br>2. Ni mambo gani tunayozingatia tunaposoma kifungu cha ufahamu? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kusoma ufahamu akiwa na wenzake.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotumia msamiati wa suala lengwa katika muktadha maalum.

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Masuala ya jinsia: mwanafunzi anaposoma matini kuhusu suala lengwa.<br>• Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kwa ufahamu katika somo la Kiswahili na stadi hiyo katika somo la English<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mitazamo hasi ya kijinsia na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Studies. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.3 Kuandika** | **5.3.1 Insha za Kiuamilifu**<br><br>*Shajara*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya shajara,<br>b) kujadili vipengele vya shajara,<br>c) kuandika shajara akizingatia vipengele vyake,<br>d) kuonea fahari matumizi ya shajara katika maisha ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya shajara,<br>• kutafiti maktabani au kusakura mtandao salama na kusoma mifano ya shajara,<br>• kujadili na mwenzake shajara aliyoisoma mtandaoni,<br>• kujadili vipengele vya shajara kwa kurejelea kielelezo cha shajara akishirikiana na wenzake,<br>• kuandika shajara akizingatia vipengele vyake kama vile mambo ya kuandika kwenye shajara, muundo na mtindo. | Kwa nini watu hutumia shajara? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadili vipengele vya shajara.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura na kusoma mtandaoni mifano ya shajara.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki kikamilifu katika mijadala kundini.

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Uadilifu: mwanafunzi anapoandika matukio ya kweli katika shajara.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anaposhiriki kikamilifu na kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini na kuheshimu maoni ya wenzake kundini. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Masuala ya jinsia: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa.<br>• Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa shajara katika somo la Kiswahili na uandishi huo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mitazamo hasi ya kijinsia na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Studies. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.4 Sarufi** | **5.4.1 Hali za Masharti**<br><br>• *Hali ya masharti* ***-nge-*** ***-ngali-***<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya hali ya masharti,<br>b) kutambua matumizi ya hali ya masharti ya **-nge-** na **-ngali-** katika matini,<br>c) kutumia hali ya masharti **-nge-** na **-ngali-** ipasavyo katika matini,<br>d) kuchangamkia matumizi yafaayo ya hali ya masharti **-nge-** na **-ngali-** ili kukuza ufasaha wa lugha. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutafiti mtandaoni au maktabani maana ya hali ya masharti,<br>• kutambua matumizi sahihi ya hali ya **-nge-** na **-ngali-**, katika sentensi au vifungu,<br>• kuchagua sentensi zinazoashiria matumizi ya hali ya **-nge-** na **-ngali-**, kutokana na mchanganyiko wa sentensi kutoka katika vitabu, tarakilishi, chati kwa kuzikolezea wino au kuzipigia mstari,<br>• kutunga sentensi kuonyesha matumizi ya hali ya **-nge-** na **-ngali-**, akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la mitazamo hasi ya kijinsia ,<br>• kutafiti matumizi ya hali **-nge-** na **-ngali-** mtandaoni na kuwawasilishia wenzake ili waitolee maoni. | Je, unapotaka kuonyesha hali ya masharti unatumia viambishi gani? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na Ushirikiano: mwanafunzi anapotoa mchango wake katika shughuli za kikundi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kutambua hali ya –**nge-** na **-ngali-**.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kwa kutumia hali ya **-nge-** na **-ngali-.**<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua hali ya **-nge-** na **-ngali-** na kuzitungia sentensi sahihi. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapovitunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Masuala ya kijinsia: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha hali ya marsharti katika somo la Kiswahili na hali hiyo katika somo la English Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mitazamo hasi ya kijinsia na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Studies. |

## 6.0 USALAMA BARABARANI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **6.1.1 Kusikiliza kwa Kufasiri**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya kusikiliza kwa kufasiri ili kuibanisha,<br>b) kueleza msimamo na mielekeo kuhusu ujumbe wa matini ya kusikiliza,<br>c) kulinganisha misimamo na mielekeo ya ujumbe wa matini aliyosikiliza na ile ya jamii yake kuhusu suala husika,<br>d) kujenga mazoea ya kutambua msimamo na mielekeo katika matini mbalimbali ili kupata maana ya ujumbe. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutafiti mtandaoni au maktabani maana ya kusikiliza kwa kufasiri na kuwasilisha matokeo ya utafiti wake darasani ili apate maoni ya wenzake,<br>• kueleza misimamo na mielekeo kuhusu ujumbe katika matini anayosikiliza kuhusu suala lengwa,<br>• kusikiliza habari kuhusu suala lengwa (miongozo kwa watumiaji wa barabara; wanaotumia usafiri wa shuleni ulioidhinishwa) katika kifaa cha kidijitali na kuchambua misimamo na mielekeo kuhusu ujumbe,<br>• kulinganisha misimamo na mielekeo kuhusu ujumbe wa matini aliyosikiliza na misimamo na mielekeo ya jamii yake kuhusu | Ni misimamo gani iliyopo katika matini ulizowahi kuzisikiliza? |



DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | suala lililozungumziwa katika matini hiyo,<br>• kutoa muhtasari wa habari aliyosikiliza kuhusu suala lengwa huku wakichanganua misimamo na mielekeo ya msimulizi /msemaji kuhusu masuala yanayozungumziwa,<br>• kuwaeleza wenzake misimamo na mielekeo kuhusu ujumbe katika matini aliyosikiliza kwa maneno yake mwenyewe na kuwataka waangazie vipengele vilivyotumiwa kuonyesha misimamo na mielekeo hiyo,<br>• kujadili na mzazi au mlezi wake kuhusu misimamo na mielekeo ya jamii yake kuhusu suala lengwa. | |

DRAFT

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadili na wenzake misimamo na mielekeo katika matini.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza habari.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapochanganua misimamo na mielekeo kuhusu ujumbe na kuihusisha na mielekeo ya jamii yake.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuwaelezea wenzake misimamo na mielekeo kuhusu ujumbe katika matini aliyosikiliza.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojadili na mzazi au mlezi wake kuhusu misimamo na mielekeo ya jamii yake kuhusu ujumbe. |
| **Maadili:**<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>• Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili kwa utulivu mielekeo na msimamo kuhusu suala linalozungumziwa. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Suala la usalama: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika kuchanganua habari kwenye matini aliyosikiliza. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusikiliza kwa kufasiri katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usalama barabarani na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies, Creative Arts and Sports na Agriculture. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.2 Kusoma** | **6.2.1 Kusoma kwa Kina**<br><br>**Ushairi**<br>• *Maudhui*<br>• *Dhamira*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya maudhui na dhamira katika fasihi,<br>b) kujadili maudhui na dhamira katika shairi,<br>c) kuchambua shairi kwa kuzingatia maudhui na dhamira,<br>d) kuchangamkia usomaji wa kina wa mashairi ili kupata ujumbe wake. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutafiti maktabani au mtandaoni maana ya maudhui na dhamira katika fasihi na kuwasilisha matokeo ya utafiti wake darasani ilia pate maoni ya wenzake,<br>• kujadili maudhui katika shairi alilosoma,<br>• kufafanua dhamira ya shairi alilosoma,<br>• kuwaelezea wenzake dhamira ya shairi alilosoma,<br>• kuchambua shairi kuhusu suala lengwa (kama vile kuhusu data ya usalama barabarani, vipengele vya ndani vya usalama wa gari) kwa kuzingatia maudhui na dhamira,<br>• kusoma mashairi katika diwani ya mashairi iliyoteuliwa na mwalimu na kuyachambua kwa kuzingatia dhamira na maudhui kisha awasilishe kazi yake kwa wenzake ili waitolee maoni. | Je, mashairi uliyowahi kuyasoma yalizungumzia nini? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapochangia kujadili maudhui na dhamira ya shairi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura kwenye mitandao salama ili kutafiti kuhusu maudhui ya ushairi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojitolea kufanya utafiti maktabani na mtandaoni.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowasilishia wenzake maudhui na dhamira ya ushairi. Haiba yake inajengeka zaidi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake wanapojadili maudhui na dhamira ya ushairi. Pia anapowakosoa wenzake kwa upole na kuthamini hoja zao.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kutafiti kuhusu maudhui na dhamira ya ushairi maktabani na mtandaoni anawajibikia majukumu aliyopewa.
- Upendo: mwanafunzi anapotoa maoni kwa heshima kuhusu uwasilishaji wa wenzake ili kuwakosoa au kuwatia motisha.

**Masuala Mtambuko:**

Masuala ya usalama: mwanafunzi anaposoma shairi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya maudhui na dhamira katika shairi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usalama barabarani na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies, Creative Arts and Sports na Agriculture.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.3 Kuandika** | **6.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>*Methali*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya insha za methali ili kuipambanua,<br>b) kujadili vipengele vya insha ya methali,<br>c) kuandika insha ya methali kwa kuzingatia vipengele vya uandishi husika,<br>d) kufurahia kufasiri methali na kuziandikia insha zinazoafiki ili kujenga ubunifu. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya insha za methali,<br>• kusoma kielelezo cha insha ya methali,<br>• kujadili na wenzake vipengele vya insha ya methali katika kielelezo cha insha aliyosoma,<br>• kuandika insha ya methali (k.v kuhusu methali zinazoangazia usalama barabarani; haraka haraka haina baraka, msafiri ni aliye pwani, polepole ndio mwendo) kwa kuzingatia vipengele vya uandishi wa insha ya methali.<br>• kuwasomea wenzake insha aliyoandika ili waitolee maoni. | Unahitaji kufanya nini unapoandika insha ya methali? |
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika kujadiliana kuhusu insha za methali.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi kuandika insha hizo za methali na kuzisambaza kwa mtandao.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapofaulu kuandika insha ya methali. | | | | |

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala ya usalama barabarani: mwanafunzi anapoandika insha ya methali kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya insha ya methali katika shairi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usalama barabarani na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies, Creative Arts and Sports na Agriculture. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.4 Sarufi** | **6.4.1 Vielezi**<br><br>• *Vielezi vya Namna*<br><br>• *Vielezi vya Wakati*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vielezi vya namna na vya wakati katika matini,<br>b) kutumia vielezi vya namna na vya wakati ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia kutumia vielezi vya namna na vya wakati katika matini. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kuchopoa vielezi vya namna na vya wakati kutoka kwenye chati, kadi maneno, kapu maneno au tarakilishi,<br>• kuvipigia mstari vielezi vya namna na vya wakati katika sentensi na vifungu,<br>• kutenga vielezi vya namna na vya wakati katika orodha ya maneno, sentensi au vifungu kwenye vitabu, tarakilishi, chati kwa kuvikolezea wino,<br>• kutunga sentensi au vifungu vifupi kwa kutumia vielezi vya namna na vya wakatiakizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la usalama barabarani,<br>• kumsomea mzazi au mlezi wake sentensi alizotunga akitumia vielezi vya namna na vya wakati. | 1. Ni vielezi vipi unavyovijua?<br>2. Vielezi huchangia vipi katika mawasiliano? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kutambua vielezi.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia vielezi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi wake sentensi alizotunga.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

Masuala ya usalama: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa akizingatia matumizi sahihi ya vielezi.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vielezi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usalama barabarani na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies, Creative Arts and Sports na Agriculture.

## 7.0 HUDUMA KATIKA ASASI ZA KIJAMII

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **7.1.1 Kusikiliza kwa Kutathmini**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya kusikiliza kwa kutathmini ili kuibainisha,<br>b) kujadili vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza kwa kutathmini,<br>c) kutathmini ujumbe wa mzungumzaji,<br>d) kutathmini mtazamo wa msemaji kuhusu anachokizungumzia,<br>e) kueleza maana ya msamiati kama ulivyotumiwa katika matini aliyosikiliza,<br>f) kuchangamkia kushiriki katika kusikiliza kwa kuchanganua ili kuboresha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya kusikiliza kwa kutathmini ili kuubainisha,<br>• kujadili na wenzake vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza kwa kutathmini kutoka kwenye mazungumzo mafupi,<br>• kusikiliza mazungumzo kuhusu suala lengwa (k.v Majukumu ya Mamlaka ya Uchukuzi na Usalama Barabarani, Kituo cha Huduma kwa Taifa,) kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au katika vifaa vya kidijitali huku akijadili vipengele vya kusikiliza kwa kutathmini vilivyozingatiwa,<br>• kutoa maoni kuhusu suala linaloshughulikiwa katika kauli au kifungu alichosikiliza,<br>• kusikiliza matini kuhusu suala lengwa kutoka kwenye kinasa | Unazingatia nini ili kupata ujumbe unaowasilishwa na mzungumzaji? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | sauti au kwa mgeni mwalikwa na kueleza maana ya msamiati ambao umetumiwa katika matini hiyo. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kujadili kuhusu vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza kwa kutathmini.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikilizia mazungumzo.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotoa mtazamo wake kuhusu suala alilosikiliza. Pia anapofasiri maana kutokana na viziada lugha kama vile ishara za uso.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia katika mazungumzo.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

Masuala ya huduma kwa jamii: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya ujifunzaji wa kusikiliza kwa kutathmini kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusikiliza kwa kutathmini katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la huduma katika asasi za kijamii na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.2 Kusoma** | **7 .2.1 Ufupisho**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya ufupisho ili kuupambanua,<br>b) kujadili vipengele vya ufupisho wa kifungu,<br>c) kufupisha kifungu akizingatia vipengele vya ufupisho,<br>d) kujenga mazoea ya kuwasiliana kwa maelezo mafupi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutafiti kuhusu maana ya ufupisho na kuwasilisha maana hiyo darasani ili wenzake waitolee maana,<br>• kutafiti na kujadili na wenzake vipengele vya kuzingatia katika kufupisha habari ya kifungu,<br>• kusoma kifungu kuhusu suala lengwa (Asasi kama vile majukumu ya Mamlaka ya Barabara ya Serikali (Bodi ya Barabara ya Kenya; Mamlaka ya Barabara za Mijini ya Kenya, Mamlaka ya Kitaifa ya Usimamizi wa Mazingira) katika matini andishi au ya kidijitali.<br>• kufupisha kifungu alichosoma kwa kuzingatia vipengele vya ufupisho,<br>• kusakura vifungu mbalimbali mtandaoni na kuvifupisha kwa kuzingatia vipengele vya ufupisho, | Je, unazingatia nini unapotaka kueleza jambo kwa ufupi? |

DRAFT

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td>• kumsomea mwenzake kifungu alichofupisha akizingatia vipengele vya ufupisho ili amtolee maoni.</td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotambua na kujadili vipengele vya kuzingatia katika kufupisha kifungu.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura vifungu mbalimbali mtandaoni na kuvifupisha.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusakura vifungu mbalimbali na kuvifupisha.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofupisha kifungu na kuwasomea wenzake.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Maadili:<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapohusishwa katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili vipengele vya kufupisha kifungu.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Masuala Mtambuko:<br>Masuala ya shughuli za huduma kwa jamii: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Uhusiano na Masomo Mengine:<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya ufupisho katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la huduma katika asasi za kijamii  na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education.</td></tr>
</table>

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.3 Kuandika** | **7.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>*Maelezo*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua lugha inayoathiri hisia mbalimbali katika insha ya maelezo,<br>b) kujadili umuhimu wa kutumia lugha inayoathiri hisia mbalimbali katika insha ya maelezo,<br>c) kutumia ipasavyo lugha inayoathiri hisia mbalimbali katika kuandika insha ya maelezo,<br>d) kufurahia kuandika insha yenye maelezo yanayojenga picha dhahiri. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua lugha inayoathiri hisi katika insha ya maelezo kutoka kwa vielelezo vya insha kwenye matini za kimaandishi au za kidijitali,<br>• kutambua jinsi matumizi ya lugha katika insha ya maelezo yanavyoathiri hisia mbalimbali,<br>• kutumia kifaa cha kidijitali kupigia mstari lugha iliyotumiwa kuathiri hisia katika kielelezo cha insha ya maelezo,<br>• kutambua umuhimu wa lugha inayoathiri hisia kutokana na kifungu kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali,<br>• kuandika insha ya maelezo kwa kuzingatia lugha inayoathiri hisia mbalimbali na kutekeleza majukumu ya kushawishi, kuburudisha, kupasha habari au kufunza.<br>• kuwasomea wenzake insha ya maelezo aliyoandika ili waitolee maoni. | Je, ni nini kinafanya maelezo katika insha kudhihirika? |

DRAFT

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kupigia mstari lugha inayoonyesha hisia.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapofaulu kuandika insha inayotumia lugha yenye kuathiri hisia za msomaji.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapowasomea wenzake insha aliyoandika ili waikosoe pamoja.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuwasomea wenzake insha aliyoandika. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala ya shughuli za huduma kwa jamii: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa insha ya maelezo katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la huduma katika asasi za kijamii na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.4 Sarufi** | **7.4.1 Vielezi**<br><br>• *Vielezi vya Mahali*<br>• *Vielezi vya Idadi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vielezi vya mahali na vya idadi katika matini,<br>b) kutumia vielezi vya mahali na vya idadi ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia kutumia vielezi vya mahali na vya idadi katika sentensi na vifungu. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kuchopoa vielezi vya mahali na vya idadi kwenye chati, kadi maneno, kapu maneno au tarakilishi,<br>• kuvipigia mstari vielezi vya mahali na vya idadi katika sentensi na vifungu,<br>• kutenga vielezi vya mahali na vya idadi katika orodha ya maneno, sentensi au vifungu kwenye vitabu, tarakilishi, chati kwa kuvikolezea wino au kuvipigia mstari,<br>• kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kutumia vielezi vya mahali na vya idadi,<br>• kutunga sentensi au vifungu kwa kutumia vielezi vya mahali na vya idadi akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la huduma katika asasi za kijamii,<br>• kuwasomea wenzake sentensi au vifungu | 1. Ni mahali gani panaweza kutajwa na vielezi vya mahali?<br>2. Ni idadi gani zinazoweza kutajwa na vielezi vya idadi? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | alivyotunga ili watambue vielezi vya mahali na vya idadi, | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzji kuhusu vielezi vya mahali na vya idadi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kutambua vielezi.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu suala lengwa akitumia vielezi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua vielezi na kuvitungia sentensi sahihi na vifungu.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomtajia mzazi au mlezi wake vielezi vinavyohusu shughuli katika mazingira ya nyumbani.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

Masuala ya huduma kwa jamii: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia vielezi.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vielezi vya mahali na vya idadi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la huduma katika asasi za kijamii na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education.

DRAFT

## 8.0 MISUKOSUKO YA KIJAMII

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **8.1.1 Uzungumzaji wa Kushawishi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya uzungumzaji wa kushawishi ili kuupambanua,<br>b) kubainisha miktadha ya uzungumzaji wa kushawishi,<br>c) kujadili vipengele vya kuzingatia katika uzungumzaji wa kushawishi,<br>d) kufanya mazungumzo ya kushawishi akizingatia vipengele vya uzungumzaji wa kushawishi,<br>e) kujenga mazoea ya kuwasilisha hoja kwa mazungumzo | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutafiti na kueleza maana ya uzungumzaji wa kushawishi,<br>• kubainisha, miktadha katika jamii yake ambamo uzungumzaji wa kushawishi hutokea,<br>• kushirikiana na wenzake kujadili vipengele vya kuzingatia katika uzungumzaji wa kushawishi,<br>• kubuni mazungumzo mepesi kuhusu suala lengwa na kuwawasilishia wenzake wamtathmini iwapo ametumia vipengele vifaavyo vya uwasilishaji wa uzungumzaji wa kushawishi,<br>• kusikiliza uzungumzaji wa kushawishi kuhusu suala lengwa kutoka kwenye kifaa | 1. Ni lini tunatumia mazungumzo ya kushawishi?<br>2. Utafanya nini ili mazungumzo yako yawe na ushawishi kwa wengine? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | yanayoshawishi hadhira. | cha kidijitali au mgeni mwalikwa na kubainisha vipengele vya uzungumzaji wa kushawishi vilivyozingatiwa,<br>• kushirikiana na wenzake katika uzungumzaji wa kushawishi kuhusu suala lengwa huku akizingatia vipengele vya uwasilishaji wa uzungumzaji wa kushawishi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojieleza kuhusu suala lengwa kwa njia wazi na kwa lugha inayomwaminisha msikilizaji kwamba anasema ukweli.
- Ubunifu: mwanafunzi anapobuni uzungumzaji wa kushawishi kuhusu suala lengwa na kuyawasilisha kwa mtindo ufaao.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kushawishi kuhusu suala lengwa.

**Maadili:**

- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake fursa ya kujieleza bila kuwakatiza au kushughulikia mengine wanapozungumza.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia katika kujifunza.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake na kutoa mchango katika shughuli za kikundi.
- Amani: mwanafunzi anaposhiriki na wengine katika mazungumzo ya kushawishi kuhusu suala lengwa kwa utulivu.

**Masuala Mtambuko:**

Suala la misukosuko ya kijamii: mwanafunzi anaposhiriki uzungumzaji wa kushawishi kuhusu suala lengwa.

DRAFT

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha uzungumzaji wa kushawishi katika somo la Kiswahili na uzungumzaji huo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la misukosuko ya kijamii na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education masuala ya kijamii.

DRAFT

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji** | **Maswali Dadisi yaliyopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **8.2 Kusoma** | **8.2.1 Kusoma kwa Kina**<br><br>**Ushairi**<br>• *Mandhari*<br>• *Muundo*<br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya mandhari katika fasihi,<br>b) kutambua mandhari mbalimbali katika shairi,<br>c) kueleza umuhimu wa mandhari katika shairi,<br>d) kufafanua vipengele vya muundo katika shairi,<br>e) kuchambua shairi kwa kuzingatia mandhari na muundo,<br>f) kuchangamkia nafasi ya mandhari na muundo katika shairi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutafiti mtandaoni au maktabani maana ya mandhari katika fasihi,<br>• kujadiliana na wenzake matokeo ya utafiti wake,<br>• kusoma mashairi mbalimbali ili kutambua mandhari mbalimbali katika shairi,<br>• kueleza umuhimu wa mandhari katika shairi,<br>• kufafanua vipengele vya muundo wa shairi ili kuipambanua<br>• kughani shairi ili kutambua mandhari na muundo katika shairi,<br>• kusoma mashairi katika diwani ya mashairi iliyoteuliwa na mwalimu na kuyachambua kwa kuzingatia mandhari na muundo | 1. Je, mashairi uliyosoma yana mandhari ya aina gani?<br>2. Vipengele vya muundo vinahusu nini? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kisha awasilishe kazi yake kwa wenzake ili waitolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotambua na kujadili mandhari na muundo kwenye shairi akiwa na wenzake katika kikundi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapochambua shairi na kubainisha mandhari na muundo wa shairi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafiti maktabani na mtandaoni kuhusu muundo na mandhari katika shairi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake wanapojadili kuhusu mandhari na muundo katika shairi.
- Upendo: mwanafunzi anapotoa maoni kuhusu uwasilishaji wa wenzake ili kuwarekebisha au kuwahimiza.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki kukariri shairi kuhusu suala lengwa.

**Masuala Mtambuko:**

Suala la misukosuko ya kijamii: mwanafunzi anaposoma shairi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya mandhari na muundo katika shairi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la misukosuko ya kijamii na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.3 Kuandika** | **8.3.1 Viakifishi**<br><br>• *Mabano*<br>• *Kistari Kifupi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya mabano na kistari kifupi katika matini,<br>b) kutumia mabano na kistari kifupi ipasavyo katika matini,<br>c) kujenga mazoea ya kutumia ipasavyo mabano na kistari kifupi katika matini ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua matumizi ya mabano na kistari kifupi katika maneno, sentensi au vifungu vya maneno kwenye matini andishi na za kidijitali,<br>• kuandika maneno, sentensi au vifungu vya maneno kuhusu suala lengwa akitumia mabano na kistari kifupi ipasavyo,<br>• kusahihisha kifungu ambacho hakijatumia mabano na kistari kifupi ipasavyo,<br>• kuandika kwenye kifaa cha kidijitali au daftarini kifungu kifupi kwa kutumia mabano na kistari kifupi ipasavyo,<br>• kuwasomea au kuwasambazia wenzake kazi yake kwenye mtandao ili waitolee maoni, | 1. Je, mabano hutumiwa vipi katika matini?<br>2. Je, kistari kifupi hutumiwa vipi katika matini? |

DRAFT

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili matumizi ya mabano na kistari kifupi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kuandika kifungu na kukisambaza mtandaoni.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapoandika vifungu vyenye matumizi yafaayo ya mabano na kistari kifupi. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Suala la misukosuko ya kijamii: mwanafunzi anapotunga sentensi au vifungu kuhusu suala lengwa akitumia mabano na kistari kifupi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha matumizi ya mabano na kistari kifupi katika somo la Kiswahili na la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la misukosuko ya kijamii na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.4 Sarufi** | **8.4.1 Ngeli na Upatanisho wa Kisarufi**<br><br>*Ngeli ya*<br>• *U-ZI*<br>• *YA-YA*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya U-ZI na YA-YA katika sentensi,<br>b) kutambua nomino za ngeli ya U-ZI na YA-YA katika matini,<br>c) kutumia nomino za ngeli ya U-ZI na YA-YA katika matini kwa kuzingatia upatanisho ufaao wa kisarufi,<br>d) kuchangamkia upatanisho ufaao wa ngeli ya U-ZI na YA-YA ili kujenga ufasaha wa lugha. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya U-ZI na YA-YA katika sentensi na mafungu ya maneno,<br>• kujaza nafasi katika sentensi au vifungu vifupi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya U-ZI na YA-YA,<br>• kuchopoa nomino za ngeli ya U-ZI na YA-YA kwenye chati, kadi maneno, kapu maneno au katika tarakilishi,<br>• kutaja majina ya vitu katika mazingira ya shuleni yaliyo katika ngeli ya U-ZI na YA-YA,<br>• kutenga nomino za ngeli ya U-ZI na YA-YA katika orodha ya nomino, sentensi au vifungu kwenye vitabu, tarakilishi, chati kwa kuzikolezea wino au kuzipigia mstari,<br>• kuunda sentensi au vifungu vifupi vyenye upatanisho ufaao wa kisarufi wa ngeli ya U-ZI na YA-YA | 1. Ni vitu gani katika mazingira yako vyenye majina yaliyo katika ngeli ya U-ZI na YA-YA?<br>2. Ni vitu gani uvijuavyo vyenye majina yaliyo katika ngeli ya U-ZI na YA -YA? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la misukosuko ya kijamii,<br>• kuwasilisha kazi yake darasani au kuwasambazia wenzake mtandaoni ili waitolee maoni,<br>• kutunga sentensi zenye upatanisho ufaao wa kisarufi wa ngeli ya U-ZI na YA-YA akitumia nomino za vitu vilivyo katika mazingira ya nyumbani, na kumsomea mzazi au mlezi wake ili amtolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotoa mchango wake katika kikundi.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi au vifungu vifupi akizingatia upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya U-ZI na YA-YA.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuunda sentensi au vifungu vifupi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya U-ZI na YA-YA.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi wake sentensi alizounda kwa kutumia nomino za ngeli ya U-ZI na YA-YA katika mazingira ya nyumbani.

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Suala la misukosuko ya kijamii: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia nomino za ngeli ya U-ZI na YA-YA. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya ngeli katika shairi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la misukosuko ya kijamii na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education. |

DRAFT

## 9.0 MATUMIZI YA VIFAA VYA KIDIJITALI KATIKA BIASHARA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **9.1.1 Kusikiliza kwa Kina**<br><br>*Sauti /**j**/ na /**nj**/*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti **/j/** na **/nj/** katika maneno,<br>b) kutamka maneno yenye sauti **/j/** na **/nj/** ipasavyo,<br>c) kubuni vitanzandimi vinavyohusisha sauti /**j** /na /**nj/,**<br>d) kuchangamkia matamshi bora ya sauti **/j/** na **/nj/** ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua sauti **/j/** na **/nj/** katika maneno,<br>• kusikiliza vitanzandimi katika kifaa cha kidijitali na kutambua maneno yenye sauti **/j/** na **/nj/** na kuyatamka ipasavyo,<br>• kutamka vitanzandimi vyepesi vinavyohusisha matamshi ya sauti/ **j/** na /**nj/**,<br>• kusikiliza vitanzandimi katika kifaa cha kidijitali na kutambua maneno yenye sauti **/j/** na **/nj/** na kuyatamka ipasavyo,<br>• kubuni vitanzandimi vinavyohusisha sauti **/j/** na **/nj/** na kuvikariri kwa wenzake,<br>• kushiriki mazungumzo na mzazi au mlezi wake kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti /**j/** na /**nj/.** | Ni maneno yapi unayoyajua yaliyo na sauti /**j**/ na /**nj**/? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua sauti **/j/** na **/nj/** katika maneno.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kusikiliza vitanzandimi vyenye sauti **/j/** na **/nj/.**<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapobuni vitanzandimi vyepesi akitumia maneno yenye sauti **/j** /na **/nj/.**<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapotamka ipasavyo sauti lengwa na anapochangia katika kazi ya kikundi.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki mazungumzo na mzazi/mlezi kwa kuhusisha matamshi bora ya sauti /**j** /na / **nj/.** |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi za kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Elimu ya matumizi ya fedha: mwanafunzi anapotamka na kutofautisha sauti lengwa katika maneno yanayohusiana na biashara. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matamshi ya sauti katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi ya vifaa vya kidijitali katika biashara na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical Studies. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.2 Kusoma** | **9.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>*Kifungu cha Kushawishi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kudondoa habari mahususi katika kifungu cha kushawishi,<br>b) kueleza maana za maneno kama yalivyotumiwa katika kifungu cha kushawishi,<br>c) kuchangamkia usomaji wa kifungu cha kushawishi ili kukuza hamu ya ujifunzaji. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kudondoa habari mahususi katika kifungu cha kushawishi,<br>• kueleza maana ya maneno kama yalivyotumika katika kifungu cha kushawishi ili kubainisha matumizi ya lugha shawishi,<br>• kutunga sentensi akitumia msamiati katika matini aliyoisoma ili kubainisha matumizi ya lugha shawishi,<br>• kujibu maswali kutokana na kifungu cha kushawishi alichokisoma,<br>• kutoa muhtasari wa kifungu cha kushawishi alichosoma na kuwasambazia wenzake mtandaoni ili wakitolee maoni,<br>• kutafiti mtandaoni kuhusu matini zinazoshughulikia suala lengwa. | Ni mambo gani unazingatia unaposoma kifungu cha kushawishi? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapohakiki sentensi zilizotungwa na wenzake kwa kutumia msamiati wa suala lengwa na kutoa maoni.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapoweza kusakura tovuti ili kutafuta matini lengwa na kuisoma kwa kuzingatia maadili.

DRAFT

Vilevile, anapoandika muhtasari kwa kutumia kifaa cha kidijitali na kuwatumia wenzake.

- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposakura mtandaoni ili kupata matini mbalimbali na kuzisoma akizingatia maadili katika usomaji wa kidijitali.
- Kujiamini: mwanafunzi anapohakiki sentensi zilizotungwa na wenzake kwa kutumia msamiati wa suala lengwa na kutoa maoni yake.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapotathmini maoni ya wenzake wanapojadili sifa zinazozingatiwa kuteua matini za kidijitali zinazofaa kusomwa. Pia anapowakosoa wenzake kwa kwa upole.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kwa kuvitunza ipasavyo na kuzingatia maadili.
- Umoja: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kujadili sifa zinazozingatiwa kuteua matini za kidijitali zinazofaa kusomwa.
- Uadilifu: mwanafunzi anapochagua matini faafu mtandaoni kwa mujibu wa sifa zinazofaa kuzingatiwa katika uteuzi wa matini husika.

**Masuala Mtambuko:**

Elimu ya matumizi ya fedha: mwanafunzi anapopata maarifa mtandaoni kuhusu matumizi ya vifaa vya kidijitali katika biashara.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha kusoma kidijitali katika somo la Kiswahili na usomaji huo katika masomo yote ya Gredi ya Tisa.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi ya vifaa vya kidijitali katika biashara na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical Studies.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.3 Kuandika** | **9.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>*Masimulizi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya ukuzaji wa wazo baina ya aya za insha ya masimulizi,<br>b) kueleza ukuzaji wa wazo baina ya aya za insha ya masimulizi,<br>c) kuandika insha ya masimulizi inayozingatia ukuzaji wa wazo baina ya aya,<br>d) kufurahia kuandika insha za masimulizi zinazozingatia ukuzaji wa wazo baina ya aya ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua vipengele vya ukuzaji wa wazo baina ya aya za insha ya masimulizi kwenye matini za kimaandishi au za kidijitali,<br>• kueleza jinsi wazo lilivyokuzwa baina ya aya za insha ya masimulizi kuandika vidokezo vya insha vinavyozingatia ukuzaji wa wazo baina ya aya,<br>• kuandika insha ya masimulizi akizingatia ukuzaji wa wazo baina ya aya na kusaidiana na wenzake kuisahihisha,<br>• kuwasomea wenzake insha aliyoandika au awasambazie kwenye vifaa vya kidijitali ili waitolee maoni,<br>• kumsomea mzazi, mlezi wake au mwenzake aya aliyoandika ili kutoa maoni. | Je, unawezaje kulikuza wazo baina ya aya za insha ya masimulizi? |

DRAFT

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika kusahihisha insha.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusambazia insha.
- Ubunifu: mwanafunzi anapolikuza wazo baina ya aya za insha katika utungo wake kwa ufasaha.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapowasomea wenzake insha aliyoandika ili waikosoe pamoja.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuandika na kuwasomea wenzake insha.

**Maadili:**
- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala Mtambuko:**
Elimu ya matumizi ya fedha: mwanafunzi anapoandika insha inayohusisha maudhui ya biashara.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa insha ya masimulizi katika somo la Kiswahili na uandishi huo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi ya vifaa vya kidijitali katika biashara na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-technical studies.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.4 Sarufi** | **9.4.1 Ngeli na Upatanisho wa Kisarufi**<br><br>*Ngeli ya*<br>• *LI*<br>• *KU*<br>• *PA-KU-MU*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU katika sentensi,<br>b) kutambua nomino za ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU katika matini,<br>c) kutumia nomino za ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU katika matini kwa kuzingatia upatanisho ufaao wa kisarufi<br>d) kuchangamkia matumizi yafaayo ya upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya PA-KU-MU katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU katika sentensi au vifungu,<br>• kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU,<br>• kuchopoa nomino za ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU kwenye chati, kadi maneno, kapu maneno au katika tarakilishi,<br>• kutaja majina ya vitu katika mazingira ya shuleni yaliyo katika ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU,<br>• kutenga nomino za ngeli LI, KU na PA-KU-MU katika orodha ya nomino, sentensi au vifungu kwenye vitabu, tarakilishi, chati kwa kuzikolezea wino au kuzipigia mstari,<br>• kutunga sentensi au vifungu vifupi vyenye upatanisho wa kisarufi ufaao wa ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU akizingatia masuala mtambuko | Ni vitu gani katika mazingira yako vyenye majina yaliyo katika ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | mbalimbali likiwemo suala la matumizi ya vifaa vya kidijitali katika biashara<br>• kumweleza mzazi, mlezi au mwenzake sentensi alizotunga akitumia nomino katika ngeli za LI, KU na PA-KU-MU ili kutoa maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu suala lengwa akitumia nomino za ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutumia nomino za ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU kuzitungia sentensi na vifungu vyenye upatanisho ufaao wa kisarufi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji, pia anapojitolea kufanya kazimradi.
- Umoja na upendo: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala Mtambuko:**

Elimu ya matumizi ya fedha: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia nomino ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya ngeli na upatanisho wa kisarufi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi ya vifaa vya kidijitali katika biashara na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-technical studies.

**10.0 KUKABILIANA NA MSONGO WA MAWAZO**

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **10.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **10.1.1 Mazungumzo**<br><br>*Malumbano ya Utani*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya malumbano ya utani kama kipera cha mazungumzo,<br>b) kujadili sifa za malumbano ya utani,<br>c) kutambua vipengele vya uwasilishaji wa malumbano ya utani,<br>d) kuwasilisha malumbano ya utani kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uwasilishaji,<br>e) kuchangamkia uwasilishaji wa malumbano ya utani kwa kuzingatia vipengele vya | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutafiti na kueleza maana ya malumbano ya utani,<br>• kutafiti na kujadili na wenzake sifa za malumbano ya utani,<br>• kutambua vipengele vya kimsingi vya uwasilishaji wa malumbano ya utani,<br>• kusikiliza malumbano ya utani katika vifaa vya kidijitali au kutoka kwa mgeni mwalikwa au mwalimu na kutambua vipengele vya kimsingi katika uwasilishaji,<br>• kuwasilisha malumbano ya utani kwa kuzingatia vipengele vya kimsingi | Malumbano ya utani huzungumzia nini? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kimsingi katika uwasilishaji. | katika uwasilishaji wake,<br>• kumweleza mzazi au mlezi jinsi ya kuwasilisha malumbano ya utani kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uwasilishaji. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapowasilisha mazungumzo kwa kuzingatia vipengele vya kimsingi vya mazungumzo.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowaeleza wenzake namna ya kuwasilisha mazungumzo.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza malumbano ya utani.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotambua vipengele vya kimsingi vya mazungumzo aliyosikiliza.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomweleza mzazi au mlezi jinsi ya kuwasilisha malumbano ya utani.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

Masuala ya afya: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake kuwasilisha malumbano ya utani kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya malumbano ya utani katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la

DRAFT

English.

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la msongo wa mawazo na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.2 Kusoma** | **10.2.1 Kusoma kwa Kina**<br><br>Ushairi<br>• *Wahusika katika shairi*<br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya wahusika katika fasihi,<br>b) kutambua wahusika katika shairi,<br>c) kujadili sifa za wahusika katika shairi,<br>d) kuchambua shairi kwa kuzingatia sifa za wahusika,<br>e) kujenga mazoea ya kuchambua wahusika katika mashairi ili kuimarisha uwazaji wa kina. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutafiti mtandaoni au maktabani maana ya wahusika katika fasihi,<br>• kutambua wahusika *(k.v. nafsineni)* katika shairi akishirikiana na wenzake,<br>• kujadili na wenzake sifa za wahusika katika shairi (jinsi ya kutambua sifa za wahusika katika shairi),<br>• kuchambua mashairi kutoka diwani iliyoteuliwa na mwalimu na kujadili sifa za wahusika kutokana na tabia zao, matendo yao, maelezo ya nafsineni kuwahusu, sura, umbo n.k,<br>• kuigiza wahusika katika mashairi ili kukuza uelewa wa sifa zao,<br>• kumsomea mzazi au mlezi wake shairi na kujadiliana naye kuhusu wahusika. | Ni wahusika gani uliokumbana nao katika mashairi uliyowahi kuya soma? |

DRAFT

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kusoma mashairi akiwa na wenzake.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kusoma mashairi kwa mahadhi yafaayo katika kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika usomaji wa shairi.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoigiza wahusika katika mashairi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapochambua wahusika katika mashairi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi mashairi na kujadiliana naye kuhusu wahusika.

**Masuala Mtambuko:**

Masuala ya afya: kutokana na ujumbe wa shairi kuhusu suala lengwa.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika majadiliano ya uchambuzi wa mashairi katika kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusoma kwa kina katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la msongo wa mawazo na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.3 Kuandika** | **10.3.1 Barua ya Kuomba Kazi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya barua rasmi ya kuomba kazi,<br>b) kutambua vipengele vya barua rasmi ya kuomba kazi,<br>c) kuandika barua rasmi ya kuomba kazi akizingatia vipengele vyake,<br>d) kujenga mazoea ya kuandika barua rasmi ya kuomba kazi ipasavyo. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya barua rasmi ya kuomba kazi,<br>• kutambua vipengele vya kimuundo vya barua rasmi ya kuomba kazi,<br>• kutambua ujumbe unaoafiki barua rasmi ya kuomba kazi kwa kujadiliana na mwenzake,<br>• kuandika barua rasmi ya kuomba kazi daftarini mwake au katika kifaa cha kidijitali na kuwasomea wenzake au kuwasambazia kupitia mtandao ili waitolee maoni,<br>• kumsomea mzazi au mlezi wake barua rasmi ya kuomba kazi aliyoandika. | Je, unazingatia nini unapoandika barua rasmi ya kuomba kazi? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika kujadili ujumbe, lugha na muundo wa barua rasmi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi kuandika barua na kuisambaza kwa mtandao.
- Ubunifu: mwanafunzi anapofaulu kuandika barua rasmi ya kuomba kazi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomwelezea mzazi au mlezi wake namna ya kuandika barua rasmi ya kuomba kazi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

Masuala ya afya: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili ujumbe, lugha na muundo wa barua rasmi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa barua rasmi katika somo la Kiswahili na uandishi huo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la msongo wa mawazo na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education.

DRAFT

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **10.4 Sarufi** | **10.4.1 Vinyume vya Vihusishi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya vinyume vya vihusishi,<br>b) kutambua vinyume vya vihusishi katika matini,<br>c) kutumia vinyume vya vihusishi ipasavyo katika matini,<br>d) kujenga mazoea ya kutumia ipasavyo vinyume vya vihusishi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya vinyume vya vihusishi,<br>• kutambua matumizi sahihi ya vinyume vya vihusishi kutoka katika vitabu, tarakilishi au chati,<br>• kuchagua sentensi zinazoashiria matumizi ya vinyume vya vihusishi kutokana na mchanganyiko wa sentensi kutoka kwenye vitabu, tarakilishi, chati kwa kuzikolezea wino au kuzipigia mstari,<br>• kujaza nafasi katika sentensi au kifungu kwa kutumia vinyume vya vihusishi ipasavyo,<br>• kuandika sentensi upya kwa kuzingatia vinyume vya vihusishi,<br>• kutunga sentensi au kifungu kifupi kuonyesha matumizi ya vinyume vya vihusishi akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la kukabiliana na msongo wa mawazo, | Kwa nini tunatumia vinyume vya vihusishi katika mawasiliano? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kumsomea mzazi, mlezi au mwenzake sentensi zenye vihusishi na vinyume vyake vinavyotokea katika mazingira ya nyumbani. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotoa mchango katika shughuli za kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kutambua vinyume vya vihusishi.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuonyesha vinyume vya vihusishi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua vinyume vya vihusishi na kuvitungia sentensi sahihi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotambua au kutunga sentensi sahihi kuhusu vinyume vya vihusishi.

**Maadili:**
- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**
Kukabiliana na msongo wa mawazo: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vinyume katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la msongo wa mawazo na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education.

DRAFT

## 11.0 HAKI ZA KIBINADAMU

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **11.1.1 Uzungumzaji katika Sherehe**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya uzungumzaji katika sherehe,<br>b) kutambua miktadha katika jamii ambapo uzungumzaji katika sherehe hufanywa,<br>c) kujadili ujumbe tofautitofauti unaoafiki uzungumzaji katika miktadha mbalimbali ya sherehe,<br>d) kujadili vipengele vya kuzingatia katika uzungumzaji katika muktadha wa sherehe,<br>e) kutoa mazungumzo | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya uzungumzaji katika sherehe,<br>• kutambua miktadha katika kijamii yake ambamo uzungumzaji katika miktadha ya sherehe hufanywa,<br>• kusakura katika mtandao kutafiti ujumbe unaoafiki uzungumzaji katika miktadha mbalimbali ya sherehe,<br>• kusikiliza uzungumzaji wa aina mbalimbali kutoka kwenye vifaa vya kidijitali, mwalimu au mgeni mwalikwa na kubainisha ule unaohusu muktadha ya sherehe,<br>• kutafiti na kujadili na wenzake vipengele vya | Ni mambo gani ya kuzingatia wakati wa kuzungumza katika muktadha wa sherehe? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | katika muktadha wa sherehe kwa kutumia vipengele vifaavyo,<br>f) kuchangamkia mazungumzo yafaayo katika miktadha ya sherehe. | kuzingatia katika kuzungumza katika miktadha ya sherehe,<br>• kuigiza uzungumzaji katika miktadha ya sherehe huku akizingatia vipengele vya uwasilishaji wa uzungumzaji wa aina hii. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapoeleza maana ya uzungumzaji katika miktadha ya sherehe.
- Ubunifu: mwanafunzi anapobuni maigizo kuhusu uzungumzaji katika miktadha ya sherehe.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kuigiza uzungumzaji katika muktadha wa sherehe akizingatia vipengele vya uwasilishaji wa uzungumzaji wa aina hii.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapojadili vipengele vya kuzingatia katika uzungumzaji katika miktadha ya sherehe.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake zamu ya kushiriki katika uzungumzaji.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapovitunza vifaa vya kidijitali alivyotumia kusakura katika mtandao kutafiti ujumbe unaoafiki uzungumzaji katika miktadha ya sherehe.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki na wengine na kuchangia katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala Mtambuko:**

Uraia: mwanafunzi anaposhiriki katika uzungumzaji kuhusu haki za binadamu.

DRAFT

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya uzungumzaji katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la haki za binadamu na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.2 Kusoma** | **11.2.1 Kusoma kwa Mapana**<br><br>*Matini ya kujichagulia*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kuteua matini ya kusoma ya kiwango chake,<br>b) kueleza ujumbe katika matini ya kujichagulia,<br>c) kutambua maana ya msamiati na matumizi mengine ya lugha katika matini ya kujichagulia,<br>d) kutumia msamiati aliojifunza ipasavyo katika sentensi,<br>e) kufurahia kusoma matini ya kujichagulia ili kujenga ufasaha wa lugha. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kuchagua matini ya kiwango chake na kuisoma,<br>• kueleza wenzake ujumbe wa matini ya kujichagulia aliyosoma,<br>• kutambua msamiati uliotumiwa katika matini ya kujichagulia,<br>• kutumia kamusi kutafuta maana ya maneno asiyoyajua,<br>• kujenga rekodi ya msamiati na matumizi mengine ya lugha aliyojifunza katika kitabu au shajara yake,<br>• kutunga sentensi akitumia msamiati katika matini aliyoisoma,<br>• kutoa muhtasari wa matini ya kujichagulia aliyosoma na kuwasilisha kwa wenzake ili waitolee maoni,<br>• kusakura mtandaoni na kujichagulia matini ya ziada kisha aisome, | 1. Unazingatia nini unapochagua matini ya kusoma?<br>2. Ni mambo gani unayoyazingatia wakati wa kusoma matini ya kujichagulia? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kumsomea mzazi au mlezi wake muhtasari wa matini ya kujichagulia aliyosoma ili amtolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapoeleza ujumbe wa matini ya kujichagulia aliyosoma.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoeleza ujumbe wa matini ya kujichagulia akizingatia ufasaha wa lugha.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotumia kwa usahihi msamiati katika matini aliyoisoma.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojichagulia matini ya kusoma na kutafuta maana za maneno asiyoyajua kwenye kamusi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura mtandaoni na kujichagulia matini ya kusoma.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapokubaliana na maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

- Masuala ya haki za binadamu: mwanafunzi anaposoma matini kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusoma kwa mapana katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la haki za binadamu na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.3 Kuandika** | **11.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>*Maelezo*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili mitazamo katika insha za maelezo,<br>b) kuandika insha ya maelezo akizingatia mtazamo mahususi,<br>c) kufurahia kuandika insha za maelezo zinazoonyesha mitazamo mahususi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua mitazamo mbalimbali ya kimaelezo katika insha za maelezo,<br>• kueleza mitazamo mbalimbali ya kimaelezo katika insha za maelezo,<br>• kuandika vidokezo vya insha vinavyozingatia mitazamo ya kimaelezo atakayotumia katika insha yake ya maelezo,<br>• kuandika insha ya maelezo akizingatia mitazamo ya kimaelezo aliyochagua kutumia,<br>• kuwasomea wenzake insha aliyoandika au awasambazie kwenye vifaa vya kidijitali ili waitolee maoni,<br>• kumsomea mzazi, mlezi au mwenzake insha ya maelezo aliyoiandika ili aitolee maoni. | Je, ni mambo gani ya kuzingatia katika kuandika insha ya maelezo? |

DRAFT

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapoandika insha na kuwasomea wenzake kwa ufasaha.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusambazia wenzake insha aliyoiandika.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha yenye mpangilio mzuri wa maelezo.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuandika insha nzuri na kuwasomea wenzake. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Masuala ya haki za binadamu: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya uandishi wa insha ya maelezo katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la haki za binadamu na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.4 Sarufi** | **11.4.1 Mnyambuliko wa Vitenzi**<br><br>*Kauli ya:*<br>• *Kutendana*<br>• *Kutendeana*<br>• *kutendesha*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vya kauli ya kutendana, kutendeana na kutendesha katika vitenzi,<br>b) kutumia vitenzi katika kauli ya kutendana, kutendeana na kutendesha ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia kutumia vitenzi katika kauli ya kutendana, kutendeana na Kutendesha ipasavyo katika matini ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua katika vitenzi, viambishi vya kauli ya kutendana, kutendeana na kutendesha,<br>• kutenga vitenzi katika kauli ya kutendana, kutendeana na kutendesha kwenye chati, kadi maneno, kapu maneno au tarakilishi,<br>• kutenga vitenzi katika kauli ya kutendana kutendeana na kutendesha katika sentensi na vifungu kwenye vitabu, tarakilishi, chati kwa kuvikolezea wino au kuvipigia mstari,<br>• kugeuza vitenzi katika kauli ya kutendana, kutendeana na kutendesha,<br>• kujaza mapengo kwa kutumia vitenzi katika kauli ya kutendana, kutendeana na kutendesha, | Kwa nini ni muhimu kujifunza kauli za vitenzi? |

DRAFT

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td><ul><li>kutunga sentensi au vifungu kwa kutumia vitenzi katika kauli ya kutendana, kutendeana na kutendesha akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la haki za kibinadamu,</li><li>kumweleza mzazi, mlezi au mwenzake jinsi ya kutumia vitenzi katika kauli ya kutendana, kutendeana na kutendesha watoe maoni yao.</li></ul></td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:<ul><li>Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kutoa mchango wake katika kazi za kikundi.</li><li>Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kutambua vitenzi katika kauli ya kutendana, kutendeana na kutendesha.</li><li>Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu suala lengwa akitumia vitenzi katika kauli ya kutendana kutendeana na kutendesha.</li><li>Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua viambishi vya kauli ya kutendana kutendeana na kutendesha na kuandika vitenzi katika kauli hizo.</li></ul></td></tr>
<tr><td colspan="5">Maadili:<ul><li>Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.</li><li>Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.</li><li>Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.</li></ul></td></tr>
</table>

DRAFT

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala mtambuko anuwai kutokana na sentensi na vifungu likiwemo suala la haki za kibinadamu. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya mnyambuliko wa vitenzi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la haki za binadamu na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education. |

DRAFT

## 12.0 MAGONJWA YANAYOTOKANA NA MIENENDO YA MAISHA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **12.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **12.1.1 Ufahamu wa Kusikiliza**<br><br>*Matini ya kusikiliza*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza habari katika matini ya kusikiliza,<br>b) kukadiria maana ya msamiati mahususi na vifungu katika matini ya kusikiliza,<br>c) kuchanganua mitazamo na maoni katika matini ya kusikiliza,<br>d) kufurahia kusikiliza matini za kusikiliza ili kupata habari mahususi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza hoja muhimu katika habari aliyosikiliza kuhusu suala lengwa kutoka kwa mwalimu, kifaa cha kidijitali, mgeni mwalikwa au wenzake,<br>• kukadiria maana ya msamiati mahususi na vifungu katika matini ya kusikiliza,<br>• kujadili na wenzake mitazamo na maoni katika kifungu cha kusikiliza,<br>• kushirikisha mzazi, mlezi au mwenzake kusikiliza kifungu kutoka kifaa cha kidijitali na kujadili mitazamo katika kifungu hicho. | Je, unazingatia nini ili kufanikisha ufahamu wa kusikiliza? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia katika mazungumzo kuhusu suala lengwa.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anaposikiliza habari, kuichanganua na kutambua hoja muhimu na kuziwasilisha kwa mtindo ufaao.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki mazungumzo na mzazi au mlezi wake kuhusu suala lengwa.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapoiwasilisha upya habari aliyosikiliza. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapowapa wengine fursa ya kutambua habari za ziada na kuzidondosha bila kuwakatiza.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia kujifunzia. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala ya afya: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika mazungumzo kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya ufahamu wa kusikiliza katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la magonjwa yanayotokana na mienendo ya maisha na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Agriculture. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **12.2 Kusoma** | **12.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kusoma kifungu kwa kuzingatia matamshi bora,<br>b) kusoma kifungu kwa kasi ifaayo,<br>c) kusoma kifungu kwa kutumia sauti ipasavyo,<br>d) kusoma kifungu kwa kuambatanisha ishara zifaazo,<br>e) kujenga mazoea ya kusoma vifungu kwa kuzingatia vipengele vya usomaji matini ufaao ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kujadiliana na wenzake vipengele vya kuzingatia katika kusoma makala kwa ufasaha,<br>• kutazama vielelezo vya video za watu wanaosoma kwa ufasaha makala akiwa na wenzake,<br>• kusoma kifungu kuhusu suala lengwa katika matini andishi au ya kidijitali akizingatia matamshi bora,<br>• kusoma kifungu kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (*maneno sahihi yasiyopungua 115 kwa dakika*),<br>• kusoma kifungu akizingatia sauti ifaayo *(k.v. kiwango cha sauti na kiimbo),*<br>• kusoma kifungu kwa kuambatanisha ishara zifaazo panapofaa,<br>• kuwasomea wenzake matini mbalimbali vitabuni au katika vifaa vya kidijitali akizingatia vipengele vya | Je, unazingatia nini unaposoma kifungu cha nathari? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | usomaji ufaao ili watoe maoni yao,<br>• kumsomea mzazi, mlezi au mwenzake kifungu akizingatia vipengele vya usomaji ufaao ili amtolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kueleza vipengele vya usomaji ufaao wa matini.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowasomea wenzake matini mbalimbali kwa kuzingatia vipengele vya usomaji bora.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kifungu akizingatia vipengele vya usomaji ufaao.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapochukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

Masuala ya afya: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusoma kwa ufasaha katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la magonjwa yanayotokana na mienendo ya maisha na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Agriculture.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **12.3 Kuandika** | **12.3.1 Hotuba ya Kushawishi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya hotuba ya kushawishi ili kuitofautisha na aina nyingine za hotuba,<br>b) kujadili vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa hotuba ya kushawishi,<br>c) kuandika hotuba ya kushawishi akizingatia vipengele vifaavyo,<br>d) kuchangamkia kuandika ipasavyo hotuba ya kushawishi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutafiti na kueleza maana ya hotuba ya kushawishi,<br>• kutambua hotuba ya kushawishi katika matini,<br>• kujadili vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa hotuba ya kushawishi,<br>• kusoma kielelezo cha hotuba ya kushawishi na kujadili na wenzake vipengele vilivyotumiwa katika hotuba hiyo,<br>• kujadili na wenzake vidokezo vinavyoweza kutumiwa katika kuandika hotuba ya kushawishi,<br>• kuandika hotuba ya kushawishi kuhusu suala lengwa akitumia vidokezo walivyovijadili,<br>• kuwasomea wenzake hotuba yake au kumsambazia kupitia mtandao ili waitolee maoni. | Unazingatia nini ili kufanya hotuba kuwa na ushawishi kwa wasomaji? |

DRAFT

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika kujadili vipengele vya kuzingatia katika kuandika hotuba ya kushawishi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kuandika hotuba ya kushawishi na kuisambaza kwa mtandao.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapoandika hotuba ya kushawishi. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapokubaliana na maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Uraia: mwanafunzi anapoandika hotuba ya kushawishi kuhusu suala lengwa.<br>• Masuala ya afya: mwanafunzi anapoandika hotuba kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya uandishi wa kiuamilifu katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la magonjwa yanayotokana na mienendo ya maisha na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Agriculture. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **12.4 Sarufi** | **12.4.1 Aina za Sentensi**<br><br>*Sentensi tata*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya sentensi tata ili kuitofautisha na aina nyingine za sentensi,<br>b) kutambua sentensi tata katika matini,<br>c) kuchambua maana mbalimbali ya sentensi tata,<br>d) kujenga ujuzi wa kuchanganua maana mbalimbali katika sentensi tata ili kufasiri habari kikamilifu. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutoa maelezo ya sentensi tata kwa usahihi,<br>• kutambua sentensi tata kwenye orodha ya sentensi kwenye vitabu, chati au tarakilishi kwa kuzipigia mstari au kuzikolezea wino,<br>• kutambua sentensi tata zinazojitokeza katika matini mbalimbali,<br>• kutolea wenzake maana tofauti za sentensi tata alizozitambua,<br>• kutunga sentensi tata kwa kuzingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la magonjwa yanayotokana na mienendo ya maisha,<br>• kuwasilisha darasani sentensi tata alizotunga ili wenzake wazitolee maoni kwa heshima na upendo,<br>• kumtungia mzazi au mlezi wake sentensi tata zinazohusu shughuli katika mazingira ya nyumbani. | Nini kinafanya sentensi kuwa tata? |

DRAFT

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi za kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutambua sentensi tata.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi tata ipasavyo.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua sentensi tata katika kifungu.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomtungia mzazi au mlezi wake sentensi tata zinazohusu shughuli katika mazingira ya nyumbani.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya aina za sentensi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la magonjwa yanayotokana na mienendo ya maisha na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Agriculture.

DRAFT

## 13.0 MSHIKAMANO WA KIJAMII

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **13 .1 Kusikiliza na Kuzungumza** | 13.1.1 **Mazungumzo**<br><br>*Mawaidha*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br><br>a) kueleza maana ya mawaidha ili kuipambanua,<br>b) kujadili ujumbe na sifa za mawaidha ya kifasihi,<br>c) kueleza vipengele vya uwasilishaji wa mawaidha,<br>d) kutambua washiriki katika mawaidha ya fasihi simulizi,<br>e) kuchambua sifa za washiriki katika mawaidha ya fasihi simulizi,<br>f) kuwasilisha mawaidha kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uwasilishaji,<br>g) kufurahia kushiriki katika | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutafiti na kueleza maana ya mawaidha,<br>• kujadili na wenzake ujumbe wa mawaidha ya kifasihi ,<br>• kujadili na wenzake sifa za mawaidha ya kifasihi,<br>• kueleza vipengele vya uwasilishaji wa mawaidha,<br>• kutambua washiriki *(fanani, hadhira*) katika mawaidha anayosikiliza,<br>• kuchambua sifa za washiriki katika mawaidha anayosikiliza kutoka kwa vifaa vya kidijitali, mgeni mwalikwa au mwalimu,<br>• kutunga mawaidha kuhusu suala lengwa na kuwawasilishia wenzake darasani,<br>• kusikiliza mawaidha atakayotolewa na mzazi au mlezi | Mawaidha hushirikisha kina nani? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | uchanganuzi wa wahusika katika tungo za fasihi simulizi. | wake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu wahusika katika mawaidha.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikilizia mawaidha.
- Ubunifu: mwanafunzi anapowatolea wenzake mawaidha.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapochanganua washiriki katika mawaidha.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowatolea wanafunzi mawaidha darasani kwa ukakamavu.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

Masuala ya kijamii: mwanafunzi anaposhiriki mawaidha kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya mazungumzo katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mshikamano wa kijamii na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education:

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **13.2 Kusoma** | **13.2.1 Kusoma kwa Kina**<br><br>*Ushairi*<br>*Mbinu za lugha*<br><br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mbinu za lugha katika fasihi,<br>b) kuchanganua matumizi ya lugha katika mashairi,<br>c) kutumia mbinu mbalimbali za lugha katika mashairi,<br>d) kuchambua shairi kwa kuzingatia mbinu mbalimbali za lugha,<br>e) kuchangamkia matumizi ya lugha katika ushairi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutafiti na kutambua mbinu za lugha katika fasihi kujadili mbinu za lugha kwa mujibu wa mashairi aliyosoma akishirikiana na wenzake,<br>• kutunga shairi jepesi (lisilozidi beti tatu) kwa kuzingatia mbinu mbalimbali za lugha na kuliwasilisha darasani,<br>• kuhakiki uwasilishaji wa wenzake kuhusu matumizi ya mbinu mbalimbali za lugha katika mashairi waliyotunga na kuyatolea maoni,<br>• kusoma mashairi katika diwani ya mashairi iliyoteuliwa na mwalimu na kuyachambua kwa kuzingatia mbinu mbalimbali za lugha kisha awasilishe kazi yake kwa wenzake ili waitolee maoni. | Matumizi ya lugha katika shairi yana umuhimi gani kwa msomaji? |

DRAFT

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki kutambua mbinu za lugha kwenye mashairi aliyosoma.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapotunga shairi jepesi.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapowasilishia wenzake shairi jepesi alilotunga akizingatia mbinu mbalimbali za lugha.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapofanya utafiti maktabani na mtandaoni kuhusu matumizi ya mbinu za lugha katika mashairi. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kujadili matumizi ya mbinu za lugha katika mashairi huku akithamini maoni yao.<br>• Upendo: mwanafunzi anapohakiki uwasilishaji wa wenzake wa mashairi huku akiwakosoa kwa upendo na kuwahimiza.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojukumika kujiandaa ipasavyo ili kuwasilishia wenzake shairi alilotunga.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kutambua mbinu mbalimbali za lugha. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala ya kijamii: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusoma kwa kina katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mshikamano wa kijamii na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **13.3 Kuandika** | **13.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>*Maelezo*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya insha ya maelezo kuhusu hali,<br>b) kutambua vipengele vya insha ya maelezo kuhusu hali,<br>c) kuandika insha ya maelezo kuhusu hali akizingatia vipengele vyake,<br>d) kufurahia kutunga insha za maelezo kuhusu hali. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kujadili dhana ya insha ya maelezo kuhusu hali akiwa na mwenzake,<br>• kujadili vipengele vya insha ya maelezo kuhusu hali akiwa na mwenzake,<br>• kutambua vipengele vya insha ya maelezo kuhusu hali katika kielelezo cha insha,<br>• kuandika insha ya maelezo inayohusu hali kutumia tarakilishi akizingatia vipengele vyake,<br>• kusomea au kumtumia mwenzake insha ya maelezo inayohusu hali kupitia mtandao ili kuitathmini,<br>• kumsomea mzazi au mlezi wake insha ya maelezo kuhusu hali aliyoandika ili atoe maoni. | Je, ni mambo gani ya kuzingatia katika kuandika insha ya maelezo kuhusu hali? |

DRAFT

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadiliana kuhusu insha ya maelezo kuhusu hali.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kuandika insha ya maelezo na kumtumia mwenzake kwa mtandao.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo kuhusu hali. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo ya hali kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya uandishi wa insha ya maelezo katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mshikamano wa kijamii na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **13.4 Sarufi** | **13.4.1 Ukanushaji**<br><br>*Hali ya masharti*<br>• *-nge-*<br>• *-ngali-*<br>• *-ki-*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua ukanushaji wa hali ya masharti -**nge-, -ngali-**, na **-ki-** katika matini,<br>b) kutumia hali ya ukanushaji wa hali ya masharti ya **-nge, -ngali-** na **-ki-** ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia matumizi sahihi ya ukanushaji wa hali ya masharti ya **-nge**, -**ngali-** na **-ki-** katika maisha ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua ukanushaji wa sentensi katika hali ya masharti ya **-nge-**, **-ngali-** na **-ki-** katika matini mbalimbali *(k.v. orodha ya sentensi, chati),*<br>• kukanusha sentensi katika hali ya masharti ya **-nge-, -ngali** na **-ki-** katika kikundi,<br>• kutunga sentensi zinazoonyesha ukanushaji wa sentensi katika hali ya masharti ya **-nge, -ngali-** na **-ki-** akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la mshikamano wa kijamii,<br>• kutumia ukanushaji wa masharti ya **-nge-, -ngali-** na **-ki** kuandika kifungu kifupi kuhusu suala lengwa,<br>• kumweleza mzazi, mlezi au mwezake namna ya kukanusha hali ya masharti ya -**nge-, -ngali-** na **-ki-** zinavyokanushwa. | Ni nini kinachoonyesha kuwa sentensi iko katika hali ya masharti? |

DRAFT

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu mada lengwa na kuwasambazia wenzake wazitolee maoni.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuonyesha ukanushaji wa hali ya masharti.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua ukanushaji wa hali ya masharti na kuutungia sentensi sahihi.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**

Masuala ya mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya ukanushaji katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mshikamano wa kijamii na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education.

DRAFT

## 14.0 MATUMIZI YA KODI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **14.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **14.1.1 Mazungumzo**<br><br>*Mawaidha*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya lugha vinavyotumika katika mawaidha,<br>b) kujadili umuhimu wa vipengele vya lugha vinavyotumika katika mawaidha,<br>c) kujadili ishara zifaazo katika kutoa mawaidha,<br>d) kutoa mawaidha kwa kuzingatia vipengele mbalimbali vya lugha ya mawaidha | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua vipengele vya lugha kwa kusikiliza mawaidha yakitolewa na mwalimu, mwanafunzi mwenzake, mgeni mwalikwa au katika vifaa vya kidijitali,<br>• kujadili umuhimu wa vipengele vya lugha vilivyotumika katika mawaidha aliyosikiliza akiwa na wenzake,<br>• kujadili na wenzake ishara zifaazo katika kutoa mawaidha,<br>• kutoa mawaidha kwa mwenzake yanayohusiana na matumizi ya ushuru akizingatia vipengele mbalimbali vya lugha,<br>• kusikiliza mawaidha yakitolewa na mzazi au mlezi wake na kutambua vipengele vya lugha katika mawaidha hayo,<br>• kusakura mtandaoni na kusikiliza mawaidha mbalimbali kisha atambue | Unazingatia nini unapotoa mawaidha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | na ishara zifaazo,<br>e) kuonea fahari utoaji wa mawaidha katika maisha ya kila siku. | vipengele vya lugha katika mawaidha hayo kumweleza mzazi, mlezi au mwenzake vipengele vya lugha ya mawaidha. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadiliana kuhusu vipengele vya lugha vilivyotumika katika mawaidha.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kiteknolojia katika kusikiliza mawaidha yakitolewa.
- Ubunifu: mwanafunzi anapomtolea mwenzake mawaidha.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kutambua vipengele vya lugha katika mawaidha. Pia anapotolea wenzake mawaidha.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi wake kusikiliza mawaidha yakitolewa mtandaoni na kutambua vipengele vya lugha vilivyotumika.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

Ujuzi wa matumizi ya fedha: mwanafunzi anapotoa mawaidha yanayohusiana na matumizi ya pesa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya mawaidha katika fasihi simulizi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika

somo la English.

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi ya ushuru na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical Studies na Religious Education.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **14.2 Kusoma** | **14.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>*Kifungu cha Mjadala*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kudondoa habari mahususi katika kifungu cha mjadala,<br>b) kueleza maana ya msamiati na vifungu kama vilivyotumiwa katika kifungu cha mjadala,<br>c) kuchanganua mitazamo katika kifungu cha mjadala,<br>d) kufurahia kusoma kwa ufahamu ili kukuza uelewa wa habari. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kudondoa habari mahususi kwa mujibu wa kifungu cha mjadala alichosoma,<br>• kusakura mtandaoni kifungu cha mjadala akisome na kudondoa habari mahususi katika kifungu hicho,<br>• kujadili na wenzake maana ya msamiati na vifungu kama vilivyotumiwa katika kifungu cha mjadala,<br>• kuchanganua mtazamo katika kifungu cha mjadala,<br>• kumweleza mzazi, mlezi au mwenzake jinsi ya kupata habari mahususi katika kifungu cha mjadala ili watoe maoni. | Ni mambo gani hujidhihirisha katika kifungu cha ufahamu? |

DRAFT

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu kifungu cha mjadala.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kiteknolojia kusakura mtandao kupata kifungu cha mjadala.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kudondoa habari katika kifungu.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma na kudondoa habari kutokana na kifungu cha mjadala.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapodondoa habari katika kifungu.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za pamoja na wengine.

**Masuala Mtambuko:**

Ujuzi wa matumizi ya fedha: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusoma kwa ufahamu katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi ya ushuru na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical Studies na Religious Education.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **14.3 Kuandika** | **14.3.1 Insha za Kiuamilifu**<br><br>*Shajara*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili umuhimu wa shajara,<br>b) kueleza aina za shajara ili kuzibainisha,<br>c) kuandika aina za shajara akizingatia vipengele vyake,<br>d) kuonea fahari matumizi ya shajara katika maisha ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutafiti na kujadili na wenzake umuhimu wa shajara,<br>• kutafiti maktabani au mtandaoni aina za shajara,<br>• kujadili na mwenzake aina za shajara alizozitafiti,<br>• kueleza vipengele vya shajara<br>• kuandika aina za shajara akizingatia vipengele vyake,<br>• kuwasomea wenzake shajara aliyoandika ili waitolee maoni. | Unazingatia nini unapoandika shajara? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadili umuhimu wa shajara.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura na kusoma mtandaoni mifano ya shajara.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki kikamilifu katika mijadala kundini.

**Maadili:**
- Uaminifu: mwanafunzi anapoandika matukio ya kweli katika shajara.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anaposhiriki kikamilifu na kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Heshima: mwanafunzi anapothamini na kuheshimu maoni ya wenzake kundini.

DRAFT

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala mtambuko mbalimbali kutokana na masuala yatakayoshughulikiwa na mwanafunzi katika shajara yake. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya uandishi wa shajara katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi ya ushuru na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical Studies na Religious Education. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **14.4 Sarufi** | **14.4.1 Udogo na Ukubwa wa Nomino**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua hali ya udogo na ukubwa katika nomino,<br>b) kutumia nomino katika hali ya udogo na ukubwa ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia kutumia kwa ufasaha nomino katika hali ya udogo na ukubwa ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aweze:<br>• kuchopoa nomino katika hali ya udogo na ukubwa kwenye chati, kadi maneno, kapu maneno au tarakilishi,<br>• kutambua viambishi vya udogo na ukubwa katika maneno,<br>• kuandika majina ya vifaa vya darasani katika udogo na ukubwa,<br>• kuambatanisha nomino za hali ya wastani na za hali ya udogo na ukubwa kwa usahihi kwenye chati za maneno,<br>• kujaza nafasi katika sentensi kwa kutumia nomino katika hali ya udogo au ukubwa,<br>• kutunga sentensi akitumia nomino katika hali ya udogo na ukubwa kwa kuzingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la matumizi ya ushuru,<br>• kumtajia mzazi au mlezi wake majina ya vifaa vya nyumbani katika udogo na ukubwa katika, mazingira ya nyumbani. | Ni maneno gani unayoyajua yaliyo katika hali ya ukubwa? |

DRAFT

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki kazi za kikundi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kiteknolojia kutambua nomino katika hali ya udogo na ukubwa.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu suala lengwa akitumia nomino katika hali ya udogo na ukubwa.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua nomino katika hali ya udogo na ukubwa na kuzitungia sentensi.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomtajia mzazi au mlezi wake nomino katika hali ya udogo na udogo katika mazingira ya nyumbani. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Ujuzi wa matumizi ya fedha: mwanafunzi anapoandika sentensi kuhusu suala lengwa kwa kutumia nomino katika hali ya udogo na ukubwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya nomino katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi ya ushuru na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical Studies na Religious Education. |

DRAFT

**15.0 MAADILI YA KITAIFA**

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **15.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **15.1.1 Kusikiliza kwa Kutathmini**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya kusikiliza kwa kutathmini,<br>b) kujadili vipengele vya kuzingatia katika kutathmini mazungumzo,<br>c) kusikiliza mazungumzo na kuyatathmini kwa kuzingatia vipengele vifaavyo,<br>d) kuchangamkia kutathmini mazungumzo ili kuimarisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutafiti na kueleza maana ya kusikiliza kwa kutathmini,<br>• kujadili na wenzake vipengele vya kuzingatia katika kutathmini mazungumzo kutoka kwenye mazungumzo mafupi,<br>• kusikiliza mazungumzo kuhusu suala lengwa kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au kwenye vifaa vya kidijitali na kuyatathmini kwa kuzingatia vipengele mbalimbali,<br>• kushiriki na mzazi au mlezi wake katika mazungumzo kuhusu suala lengwa na kutoa maoni kuhusu suala linalozungumziwa. | 1. Kusikiliza kwa kutathmini mazungumzo kuna umuhimu gani?<br>2. Unazingatia nini katika kutathmini ufaafu wa mazungumzo? |

DRAFT

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia katika kujadili kuhusu vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza kwa kutathmini.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikilizia mazungumzo kuhusu suala lengwa na kutathmini.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotathmini yaliyozungumziwa na kutoa uamuzi kuhusu vipengele ambavyo vimetumiwa.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofanikiwa kutoa mtazamo wake kuhusu suala linalozungumziwa katika mazungumzo aliyoyasikiliza.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki mazungumzo kuhusu suala lengwa na mzazi au mlezi wake na kujifunza zaidi vipengele vya kusikiliza kwa kutathmini.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoyathamini maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

Maadili ya kitaifa: mwanafunzi anaposhirikiana wenzake katika mazungumzo kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya aina za uzungumzaji katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la maadili ya kitaifa na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **15.2 Kusoma** | **15.2.1 Ufupisho**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili vipengele vya kuzingatia katika ufupisho wa habari katika matini,<br>b) kuandika ufupisho wa habari kwa kuzingatia vipengele vifaavyo,<br>c) kufurahia kufupisha habari kwa usahihi katika miktadha mbalimbali. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kujadili na wenzake vipengele vya ufupisho wa habari katika matini *(kuzingatia maelekezo ya ufupisho, kueleza habari upya kwa maneno yake mwenyewe, kudondosha mifano na maelezo ya ziada, mpangilio wenye muwala),*<br>• kuandika ufupisho wa habari kwa kuzingatia vipengele vifaavyo na kuwasomea wenzake ili watoe maoni yao,<br>• kusoma matini mbalimbali zikiwemo za mtandaoni na kufupisha habari kwa usahihi,<br>• kumsomea mzazi, mlezi au mwenzake habari aliyoifupisha kutoka katika matini aliyoisoma ili aitolee maoni. | Unazingatia nini ili kuandika ufupisho ufaao? |
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu vipengele vya kuzingatia katika ufupisho wa habari. | | | | |

DRAFT

- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kusoma makala.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoeleza kwa kifupi makala aliyosoma.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma makala kutoka mtandaoni na kuyafupisha ipasavyo.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

Maadili ya kitaifa: mwanafunzi anaposoma na kufupisha habari katika matini kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya ufupisho katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la maadili ya kitaifa na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **15.3 Kuandika** | **15.3.1 Kujibu Baruapepe**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili vipengele vya kuzingatia katika kujibu baruapepe,<br>b) kujibu baruapepe kwa kuzingatia vipengele vifaavyo,<br>c) kujenga mazoea ya kujibu baruapepe ipasavyo. | Mwanafunzi aweze:<br>• kujadili na wenzake vipengele vya kuzingatia katika kujibu baruapepe,<br>• kutambua na kutumia lugha inayofaa kwa uandishi wa barua ya kujibu baruapepe,<br>• kujadili na wenzake vidokezo vya kutumia katika kujibu baruapepe,<br>• kuandika barua baruapepe kuhusu suala lengwa kwenye tarakilishi na kuwasambazia wenzake kupitia mtandao,<br>• kumweleza mzazi, mlezi au mwenzake namna ya kujibu baruapepe ili waitolee maoni. | 1. Je, ni mambo gani ya kuzingatia unapoandika baruapepe?<br>2. Je, ni mambo gani ya kuzingatia katika kujibu baruapepe? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu vipengele vya kuzingatia katika kujibu baruapepe.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kuandika baruapepe na kuisambazia wenzake.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika baruapepe ipasavyo.

DRAFT

- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomwelezea mzazi au mlezi wake namna ya kujibu baruapepe.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

Maadili ya kitaifa: mwanafunzi anapoandika baruapepe kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya uandishi wa kidijitali katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la maadili ya kitaifa na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **15.4 Sarufi** | **15.4.1 Usemi Halisi** na **Usemi wa Taarifa**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili kanuni za kubadilisha usemi halisi kuwa usemi wa taarifa,<br>b) kutumia usemi halisi na usemi wa taarifa ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia matumizi ya usemi halisi na usemi wa taarifa katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aweze:<br>• kujadiliana na wenzake kanuni za kubadilisha usemi halisi kuwa usemi wa taarifa,<br>• kugeuza sentensi zilizo katika usemi halisi ziwe katika usemi wa taarifa,<br>• kugeuza sentensi zilizo katika usemi wa taarifa ziwe katika usemi halisi,<br>• kushiriki katika mchezo wa kuchopoa kadi katika vikundi. Kikundi kimoja kichopoe kadi ya sentensi sahili katika usemi halisi na kikundi kingine kichopoe sentensi hiyo katika usemi wa taarifa,<br>• kutunga sentensi sahili katika usemi halisi na usemi wa taarifa daftarini mwake kwa kuzingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala maadili ya kitaifa,<br>• kumsomea mzazi, mlezi au mwenzake sentensi sahili alizotunga za usemi halisi | 1. Usemi halisi unatofautianaje na usemi wa taarifa?<br>2. Unazingatia nini unapoandika usemi halisi?<br>3. Unazingatia nini unapoandika usemi wa taarifa? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | na usemi wa taarifa ili kuzitolea maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi na kujadili kuhusu usemi halisi na usemi wa taarifa.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahili za usemi halisi na usemi wa taarifa.
- Kujiamini: mwanafunzi anapomsomea mwenzake sentensi sahili alizotunga za usemi halisi na usemi wa taarifa.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

- Maadili ya kitaifa: mwanafunzi anapotumia usemi halisi na usemi wa taarifa kuhusu suala lengwa.
- Masuala mtambuko mbalimbali kulingana na sentensi zilizotungwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya usemi halisi na usemi wa taarifa katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la maadili ya kitaifa na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education.

DRAFT

## MWONGOZO WA VIGEZO NA VIWANGO VYA KUTATHMINIA ULIOPENDEKEZWA

| **MADA: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| **Kuweza kusikiliza na kujibu ipasavyo** **(***Mjadala, maagizo, kusikiliza kwa kutathmini, kusikiliza kwa makini*) | Anasikiliza na kujibu ipasavyo akizingatia aina mbalimbali za kusikiliza na kujibu kwa wepesi. | Anasikiliza na kujibu ipasavyo akizingatia aina mbalimbali za kusikiliza na kujibu. | Anasikiliza na kujibu ipasavyo akizingatia baadhi ya aina za kusikiliza na kujibu. | Anasikiliza na kujibu ipasavyo akizingatia baadhi ya aina za kusikiliza na kujibu kwa kuelekezwa. |
| **Kusikiliza kwa kina** (*Matamshi ya sauti mbalimbali: /b/, /mb/, /j/, /nj/)* | Anasikiliza na kutambua sauti lengwa na kuzitamka kwa ufasaha. | Anasikiliza na kutambua sauti lengwa na kuzitamka. | Anasikiliza na kutambua baadhi ya sauti lengwa na kuzitamka. | Anasikiliza na kutambua baadhi ya sauti lengwa na kuzitamka akiongozwa. |
| **Kuweza kusikiliza na kufasiri ujumbe** *(Kufasiri ujumbe, kueleza msimamo na mielekeo kuhusu ujumbe)* | Anasikiliza, kufasiri na kueleza msimamo na mielekeo kuhusu ujumbe kwa utendeti. | Anasikiliza, kufasiri na kueleza msimamo na mielekeo kuhusu ujumbe. | Anasikiliza, kufasiri na kueleza msimamo na mielekeo kuhusu ujumbe kwa kiasi. | Anasikiliza, kufasiri na kueleza msimamo na mielekeo kuhusu ujumbe kwa kiasi akielekezwa. |

DRAFT

| **MADA: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| **Kuweza kuzungumza na kujieleza kwa ufasaha** (*Uzungumzaji wa kushawishi, uzungumzaji katika sherehe)* | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akizingatia aina mbalimbali za uzungumzaji kwa ubunifu. | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akizingatia aina mbalimbali za uzungumzaji. | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akizingatia baadhi ya aina za uzungumzaji. | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akizingatia baadhi ya aina za uzungumzaji akielekezwa. |
| **Kuweza kuwasilisha ujumbe na fani katika tungo za fasihi.** *(Semi – [tashbihi, sitiari, methali, vitendawili, nahau], Mazungumzo [malumbano ya utani, Mawaidha])* | Anawasilisha ujumbe na fani katika tungo mbalimbali za fasihi kwa ubunifu. | Anawasilisha ujumbe na fani katika tungo mbalimbali za fasihi. | Anawasilisha ujumbe na fani katika baadhi ya tungo za fasihi. | Anawasilisha ujumbe na fani katika baadhi ya tungo za fasihi kwa kusaidiwa. |

DRAFT

| MADA: KUSOMA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| **Kuweza kusoma kwa ufahamu – Vifungu mbalimbali k.v. simulizi, mjadala, shawishi** *(ujumbe na msamiati)* | Anasoma vifungu vya aina mbalimbali na kutambua ujumbe na msamiati kwa utendeti. | Anasoma vifungu vya aina mbalimbali na kutambua ujumbe na msamiati. | Anasoma baadhi ya vifungu na kutambua ujumbe na msamiati. | Anasoma baadhi ya vifungu na kutambua ujumbe na msamiati kwa kiasi. |
| **Kuweza kusoma kwa kina.** *(Ushairi: maudhui, dhamira, mandhari, ploti, wahusika, mbinu za lugha)* | Anasoma mashairi na kutambua maudhui, dhamira, mandhari, ploti, wahusika na mbinu za lugha kwa utendeti. | Anasoma mashairi na kutambua maudhui, dhamira, mandhari, ploti, wahusika na mbinu za lugha. | Anasoma mashairi na kutambua baadhi ya yafuatayo; maudhui, dhamira, mandhari, ploti, wahusika na mbinu za lugha | Anasoma mashairi na kutambua baadhi ya yafuatayo; maudhui, dhamira, mandhari, ploti, wahusika na mbinu za lugha kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kusoma kwa ufasaha.** (*Matamshi bora, kiwango kifaacho cha sauti, kasi ifaayo, ishara zifaazo*) | Anasoma kwa kuzingatia vipengele vya kusoma kwa ufasaha kina. | Anasoma kwa kuzingatia vipengele vya kusoma kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya kusoma kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya kusoma kwa ufasaha kwa kuelekezwa. |

DRAFT

| MADA: KUSOMA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Viwango / Vigezo | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| **Kuweza kusoma kwa mapana.** *(Kutambua na kuchagua matini ya kusoma*, *kutambua ujumbe, msamiati na matumizi ya lugha)* | Anasoma matini ya kujichagulia na kutambua ujumbe na matumizi ya lugha kwa mapana. | Anasoma matini ya kujichagulia na kutambua vipengele vinavyozingatiwa. | Anasoma matini ya kujichagulia na kutambua baadhi ya vipengele vinavyozingatiwa. | Anasoma matini ya kujichagulia na kutambua baadhi ya vipengele vinavyozingatiwa kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kutambua vipengele vya ufupisho na kufupisha matini.** | Anatambua vipengele vya ufupisho na kufupisha matini kwa utendeti. | Anatambua vipengele vya ufupisho na kufupisha matini. | Anatambua baadhi ya vipengele vya ufupisho na kufupisha matini. | Anatambua baadhi ya vipengele vya ufupisho na kufupisha matini kwa kuongozwa. |

DRAFT

| **MADA: KUANDIKA** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Viwango**<br>**Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| **Kuweza kutumia viakifishi mbalimbali** *(Koloni, nusu koloni, mabano, kistari kifupi)* | Anatumia alama ya koloni, nusu koloni, mabano, kistari kifupi kikamilifu na kwa wepesi. | Anatumia alama ya koloni, nusu koloni, mabano, kistari kifupi kikamilifu. | Anatumia baadhi ya za kuakifisha mshazari kikamilifu. | Anatumia baadhi ya alama za kuakifisha kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kuandika aina mbalimbali za insha za kubuni.** (*masimulizi, maelezo, mdokezo)* kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo: muundo, ujumbe, mtindo na kanuni zifaazo za uandishi. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uandishi kwa utendeti. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uandishi. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vifaavyo vya uandishi. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vifaavyo vya uandishi kwa kuongozwa. |
| **Kuweza kuandika aina mbalimbali za insha za kiuamilifu.** (*Kujibu barua ya kirafiki, shajara, barua ya kuomba kazi, hotuba ya kushawishi, kujibu* | Anaandika aina mbalimbali za insha za kiubunifu kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uandishi kwa | Anaandika aina mbalimbali za insha za kiubunifu kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya | Anaandika baadhi ya insha za kiubunifu kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vifaavyo vya uandishi. | Anaandika baadhi ya insha za kiubunifu kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vifaavyo vya uandishi kwa kuongozwa. |

| MADA: KUANDIKA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Viwango<br>Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| *baruapepe ya kiofisi)* kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo: muundo, ujumbe, mtindo na kanuni zifaazo za uandishi. | utendeti. | uandishi. | | |

DRAFT

| MADA: SARUFI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| **Kuweza kutambua na kutumia aina mbalimbali za maneno katika lugha ya Kiswahili.**<br>(*Aina mbalimbali za vihusishi na vielezi)* | Anatambua na kutumia aina mbalimbali za maneno katika lugha ya Kiswahili kwa uketo. | Anatambua na kutumia aina mbalimbali za maneno katika lugha ya Kiswahili. | Anatambua na kutumia baadhi ya aina za maneno katika lugha ya Kiswahili. | Anatambua na kutumia baadhi ya aina za maneno katika lugha ya Kiswahili kwa kuelekezwa. |
| **Kuweza kutambua na kutumia viambishi vya nyakati na hali katika vitenzi.**<br>(*Hali ya kufuatana kwa vitendo-kiambishi 'ka'; Hali za Masharti (-ki-),* | Anatambua na kutumia viambishi vya nyakati na hali katika vitenzi kwa uketo. | Anatambua na kutumia viambishi vya nyakati na hali katika vitenzi. | Anatambua na kutumia baadhi ya viambishi vya nyakati na hali katika vitenzi. | Anatambua na kutumia baadhi ya viambishi vya nyakati na hali katika vitenzi kwa kuelekezwa. |

DRAFT

| MADA: SARUFI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| **Kuweza kutambua viambishi vya ngeli, ngeli za nomino na kutumia upatanisho wa kisarufi ipasavyo.** *(U-ZI, YA-YA, LI, KU, PA-KU-MU)* | Anatambua viambishi vya ngeli, ngeli za nomino na kutumia upatanisho wa kisarufi ipasavyo na kwa utendeti. | Anatambua viambishi vya ngeli, ngeli za nomino na kutumia upatanisho wa kisarufi ipasavyo. | Anatambua baadhi ya viambishi vya ngeli, ngeli za nomino na kutumia upatanisho wa kisarufi ipasavyo. | Anatambua baadhi ya viambishi vya ngeli, ngeli za nomino na kutumia kwa kiasi upatanisho wa kisarufi ipasavyo. |
| **Kuweza kutambua vinyume vya vihusishi na kuvitumia katika matini.** | Anatambua vinyume vya vihusishi na kuvitumia katika matini kwa ubunifu. | Anatambua vinyume vya vihusishi na kuvitumia katika matini. | Anatambua vinyume vya baadhi ya vihusishi na kuvitumia katika matini. | Anatambua vinyume vya baadhi ya vihusishi na kuvitumia katika matini kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kutambua na kutumia vitenzi katika kauli mbalimbali.** *(Kutendana,* | Anatambua na kutumia vitenzi katika kauli mbalimbali kwa wepesi. | Anatambua na kutumia vitenzi katika kauli mbalimbali. | Anatambua na kutumia vitenzi katika baadhi ya kauli. | Anatambua na kutumia vitenzi katika baadhi ya kauli kwa kusaidiwa. |

DRAFT

| MADA: SARUFI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| *kutendeana, kutendesha)* | | | | |
| **Kuweza kutambua na kutumia sentensi tata.** | Anatambua na kutumia sentensi tata katika matini kwa uketo. | Anatambua na kutumia sentensi tata katika matini. | Anatambua na kutumia baadhi ya sentensi tata katika matini. | Anatambua na kutumia baadhi ya sentensi tata katika matini kwa kuelekezwa. |
| **Kuweza kutambua maneno yaliyokanushwa, viambishi vya ukanushaji na kukanusha maneno kwa kuzingatia hali ya masharti -nge-, -ngali-, -ki-.** | Anatambua maneno yaliyokanushwa, viambishi vya ukanushaji na kukanusha kwa kuzingatia hali ya masharti -nge-, -ngali- na -ki- ipasavyo na kwa wepesi. | Anatambua maneno yaliyokanushwa, viambishi vya ukanushaji na kukanusha kwa kuzingatia hali ya masharti -nge-, -ngali- na -ki- ipasavyo. | Anatambua maneno yaliyokanushwa, viambishi vya ukanushaji na kukanusha kwa kiasi kwa kuzingatia hali ya masharti -nge-, -ngali- na -ki- ipasavyo. | Anatambua maneno yaliyokanushwa, viambishi vya ukanushaji na kukanusha kwa kiasi kwa kuzingatia hali ya masharti -nge-, -ngali- na -ki- kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kutambua na kutumia nomino** | Anatambua na kutumia nomino katika hali ya | Anatambua na kutumia nomino katika hali ya | Anatambua na kutumia baadhi ya nomino katika | Anatambua na kutumia baadhi ya nomino katika |

DRAFT

| MADA: SARUFI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| **katika hali ya ukubwa na udogo.** | ukubwa na udogo kwa ufasaha. | ukubwa na udogo. | hali ya ukubwa na udogo. | hali ya ukubwa na udogo akielekezwa. |
| **Kuweza kutumia usemi halisi na usemi wa taarifa.** | Anatumia usemi halisi na usemi wa taarifa katika matini kikamilifu kwa wepesi. | Anatumia usemi halisi na usemi wa taarifa katika matini kikamilifu | Anatumia kwa kiasi usemi halisi na usemi wa taarifa katika matini kikamilifu. | Anatumia kiasi usemi halisi na usemi wa taarifa katika matini kwa kuongozwa. |

DRAFT

## KAZI MRADI YA SHUGHULI YA HUDUMA YA KIJAMII INAZOCHANGIA UJIFUNZAJI

**Utangulizi**

Katika Gredi ya Tisa, wanafunzi watashiriki katika mradi wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji kwa kuchagua kutoka somo moja au kwa kuunganisha masomo mbalimbali. Mradi wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji utamwezesha mwanafunzi kutumia maarifa na ujuzi kutoka masomo mengine kushughulikia tatizo katika jamii. Utekelezaji wa mradi huu wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji utachukua Mtazamo Kamili wa Shule, ambapo wanachama wote wa jamii ya shule ikiwa ni pamoja na walimu, utawala wa shule, wazazi/walezi/ jamii na wafanyakazi wengine wa shuleni. Itakuwa jitihada za ushirikiano ambapo mwalimu wa Somo la Kijamii (naratibu na kufanya kazi na walimu wengine wa masomo mbalimbali kubuni na kutekeleza miradi ya shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji pamoja. Walimu watachagua mada kutoka kwa masomo mbalimbali na mada tofauti tofauti za masuala mtambuko kwa mradi wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji. Pia inapaswa kutoa fursa ya ukuzaji wa umilisi wa kimsingi na maadili. Wanafunzi watashiriki katika mradi mmoja wa pamoja wa darasa wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji ulioounganishwa ukifuata hatua 6 za maendeleo kama ifuatavyo:

| Hatua | Maelezo |
|---|---|
| **Hatua ya 1** | **Utambuzi wa Tatizo**<br>Wanafunzi wanachunguza jamii yao ili kuelewa changamoto zinazokabiliwa na athari zake kwa wanajamii. Baadhi ya changamoto katika jamii zinaweza kuwa:<br>● Uharibifu wa mazingira<br>● Magonjwa ya mienendo ya maisha, magonjwa ambukizi na yasiyoambukizwa<br>● Umaskini<br>• Misukosukona migogoro katika jamii |

DRAFT

| | |
|---|---|
| | • Uhifadhi wa vyakula |
| **Hatua 2** | **Kubuni Suluhisho**<br>Wanafunzi wanabuni njia ya kuingilia kati kushughulikia changamoto iliyotambuliwa. |
| **Hatua 3** | **Mpango wa Mradi**<br>Wanafunzi wanagawana majukumu, kutengeneza orodha ya shughuli zitakazofanywa, kuandaa rasilimali zinazohitajika kwa ajili ya kutekeleza mradi, na kuweka ratiba za utekelezaji. |
| **Hatua 4** | **Utekelezaji**<br>Wanafunzi wanatekeleza mradi na kuweka idhibati wa kazi iliyofanywa. |
| **Hatua 5** | **Kuonyesha Mradi na Kuandika Ripoti**<br>Maonyesho ni pamoja na kuonyesha vitu vya mradi wa wanafunzi kwa jamii na kutafakari kuhusu maoni wanayopokea.<br>Wanafunzi wanandika ripoti inayoelezea shughuli za mradi wao na mafunzo waliyopata kutokana na maoni waliyopewa. |
| **Hatua 6** | **Tafakuri**<br>Wanafunzi wanapitia kazi yote ya mradi kujifunza kutokana na changamoto walizokutana nazo. Wanahusisha kazi ya mradi na dhana za masomo, wakiangazia jinsi dhana hizo ziliwasaidia kutekeleza mradi pamoja na jinsi mradi ulivyosaidia kuimarisha uelewa wao wa dhana za masomo. |

**Tanbihi**: Hatua hizi zitapangwa kwa muda katika mihula mitatu ya kalenda ya masomo.

DRAFT

**Tathmini ya miradi ya shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji (CSL)**

Tathmini kwa ajili ya mradi wa CSL uliounganishwa utafanywa kwa njia ya tathmini ya mara kwa mara. Tathmini itazingatia mchakato na matokeo ya mwisho. Hii inajumuisha kutathmini kila hatua ya maendeleo ya mradi wa darasa wa CSL. Itatazama vipengele vitatu, yaani: ujuzi kutoka masomo mbalimbali uliotumika katika kutekeleza mradi, umilisi wa kimsingi uliokuzwa, na maadili yaliyokuzwa.

DRAFT

**MUHTASARI WA MBINU ZA KUTATHMINI, NYENZO ZA KUFUNDISHIA NA MAPENDEKEZO YA SHUGHULI NYINGINE ZILIZORATIBIWA ZA UJIFUNZAJI**

| **Mada** | **Mapendekezo ya Mbinu za Kutathmini** | **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia** | **Mapendekezo ya Shughuli Nyingine Zilizoratibiwa za Ujifunzaji** |
|---|---|---|---|
| **Kusikiliza na Kuzungumza** | a) Kumakinikia jinsi mwanafunzi anavyotumia lugha katika mawasiliano<br>b) Kujibu maswali<br>c) Maigizo<br>d) Kutambua k.m. kwenye orodha<br>e) Kuambatanisha maneno na majibu<br>f) Mijadala<br>g) Mazungumzo<br>h) Matumizi ya ishara za mwili k.v ishara za uso, za mikono na mabega kuimarisha masimulizi yake<br>i) Wanafunzi kufanyiana tathmini | • Chati<br>• Michoro na picha<br>• Mgeni mwalikwa<br>• Vifaa vya kidijitali (k.v. tarakilishi/vipakatalishi, kinasasauti, rununu, projekta, video)<br>• Mti maneno<br>• Kapu maneno<br>• Vitabu mbalimbali | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |
| **Kusoma** | a) Kutunga sentensi k.m. kwa kutumia msamiati lengwa<br>b) Kujibu maswali k.m. katika | • Tarakilishi/vipakatalishi<br>• Kinasasauti<br>• Rununu | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala |

DRAFT

| | | | |
|---|---|---|---|
| | ufahamu<br>c) Kutoa muhtasari wa ufahamu au matini yaliyosomwa<br>d) Kusoma kwa sauti<br>e) Wanafunzi kufanyiana tathmini<br>f) Potifolio<br>g) Shajara | • Projekta<br>• Tarakilishi/vipakatalishi<br>• Kinasasauti<br>• Rununu<br>• Kamusi mbalimbali | mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |
| **Kuandika** | a) Kuandika tungo mbalimbali<br>b) Wanafunzi kufanyiana tathmini<br>c) Potifolio<br>d) Shajara<br>e) Mijadala kuhusu vidokezo vya insha | • Kielelezo cha insha ya masimulizi<br>• Kielelezo cha insha ya maelezo<br>• Kielelezo cha insha ya wasifu<br>• Nakala ya barua ya kirafiki<br>• Nakala ya barua rasmi | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |
| **Sarufi** | a) Kutambua k.m. kwenye orodha<br>b) Kuambatanisha maneno lengwa<br>c) Kujaza mapengo<br>d) Kutunga sentensi<br>e) Kazi mradi | • Tarakilishi/vipakatalishi<br>• Kinasasauti<br>• Rununu<br>• Projekta<br>• Kapu maneno<br>• Mti maneno<br>• Kadi maneno<br>• Picha za vitu mbalimbali<br>• Michoro | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Ziara za nyanjani<br>4. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |

DRAFT

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | • Chati<br>• Mabango<br>• Sanamu<br>• Nyenzo halisi | |

DRAFT